# Nipashe

Ijumaa Februari 21, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580160

www.ippmedia.com

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Wanafunzi 206 wapata ujauzito wilaya mbili ndani ya mwaka

UKURASA 3




UKURASA 13

# Mbowe: Tunawafahamu wote wanaotaka kuhama Chadema

UKURASA 2




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi, Biashara Ndogo na Kati wa Benki ya NMB, Fibert Mponzi (kushoto), na Kamishna wa Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Bima nchini (TIRA), Dk. Musa Juma (kulia), wakizindua NMB BancAssurance ambayo itakuwa inatoa huduma za bima katika matawi yote ya benki ya NMB nchini katika sherehe zilizofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mjumbe wa Bodi ya benki hiyo, Margaret Ikongo na Meneja wa Usimamizi wa Fedha BoT, Mussa Sadat. PICHA: SELEMANI MPOCHI

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**WAZIRI MKUU AFUNGUKA VITAMBULISHO VYA TAIFA**
WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema hatua ya Serikali kuagiza umakini ...

UKURASA WA 8

**SIKU ZAONGEZWA UBORESHAJI DAFTARI LA WAPIGAKURA DAR**
TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imeongeza muda wa siku tatu katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu...

UKURASA WA 3

**HATIMA YA LISSU KUKAMATWA LEO**
MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imepanga leo kusikiliza maombi ya wadhamini Ibrahim Ahmed na Robart





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# JPM asikia kilio cha madaktari



UKURASA 2

## WANAFUNZI 1,000 KWA MATUNDU 3 YA VYOO

UKURASA 18


MICHEZO YANGA YAICHAMBUA COASTAL UK. 28

MAONI, KATUNI UK.4

# Mbowe: Tunawafahamu wote wanaotaka kuhama Chadema

**Na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, amesema chama hicho kinawafahamu makada wa chama hicho wenye mipango ya kutengeneza migogoro na baadaye kuhama.

Hata hivyo, kiongozi huyo wa Chadema amesema hawawezi kuwafukuza katika chama hicho hadi pale watakapoamua kuondoka wenyewe.

Mbowe aliyasema hayo jana alipohojiwa kuhusu makada wa Chadema waliokihama chama hicho na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi hivi karibuni.

Kiongozi huyo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, alidai makada wa chama hicho waliotimkia CCM hivi karibuni, ni majeruhi wa uchaguzi wa ndani ya chama hicho uliofanyika mwishoni mwa mwaka jana na baadhi yao kushindwa kutetea nafasi zao.

"Tunatambua watu ambao wanatengenezwa ili wazue migogoro ndani ya chama chetu, na tunatambua watu ambao wakati wowote wakikamilisha malengo waliyopewa, wataondoka.

"Hatuwezi kuwafukuza kwa sababu hata tukiwafukuza, baadaye watapiga kelele tumefukuzwa... tumefukuzwa... tumeonewa... tumeonewa! Tunawaacha waondoke wenyewe kwa utashi wao," alisema.

Alisema sababu zinazotolewa na makada hao kwa sasa hazina mashiko kwa kuwa chama kinatambua kuondoka kwao kunasukumwa na matokeo ya majeraha waliyoyapata katika uchaguzi wa ndani ya chama hicho na si rahisi kuwazuia.

"Wote hao walipoingia, walitoa kauli nzito nzito, lakini katika kipindi cha miaka mitatu, minne, wanatoka wanakimbia sasa. Leo wakitoka wanapiga kelele, haiwasaidii," alisema.

Mwanzoni mwa wiki, aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vicent Mashinji, alikihama Chadema na kujiunga na CCM, akidai chama hicho kikuu cha upinzani nchini hakina uwezo wa kuwaletea maendeleo wananchi na kimekuwa na malumbano na migogoro ya ndani.

Dk. Mashinji alitangaza uamuzi huo ikiwa ni siku chache baada ya aliyekuwa mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Chadema katika uchaguzi uliopita, Cecil Mwambe, kutangaza mwishoni mwa wiki kujiuzulu ubunge wa Ndanda na uanachama wa Chadema na kujiunga na CCM.

Vigogo wengine walioihama Chadema na kurejea CCM walikotoka ni mawaziri wakuu wastaafu, Edward Lowassa na Frederick Sumaye.



Rais John Magufuli akihutubia wakati wa maadhimisho ya Siku ya Madaktari Kitaifa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# JPM asikia kilio cha madaktari

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli, amesikia kilio cha madaktari nchini baada ya jana kuagiza 1,000 waajiriwe mara moja ili kutatua tatizo la ajira kwa kada hiyo.

Vilevile, ameeleza kutofurahishwa na vitendo vya baadhi ya wanasiasa kuwanyanyasa madaktari na watumishi wengine wa sekta ya afya kwa kuwaweka ndani bila kufuata taratibu zilizowekwa kisheria.

Rais Magufuli alitangaza neema hiyo jana, wakati akizungumza na watumishi wa afya katika Mkutano wa Chama cha Madaktari (MAT) uliofanyika jijini Dar es Salaam.

"Kama mambo yatanyooka katika siku za usoni, tutaangalia hizi 'benefits' (stahiki) zenu ambazo mmezieleza hapa, sioni huo moyo wa kuzuia, siuoni," alisema.

Rais Magufuli alieleza kuwa walishindwa kuwalipa stahiki zao kutokana na kulazimika kununua vifaa vya matibabu vya kutosha nchini ili Watanzania wapate matibabu nchini badala ya kwenda kutibiwa ughaibuni.

"Nafahamu bado kuna madaktari 2,700 ambao hawajaajiriwa, hili nalifanyia kazi, nafikiri tunaweza tukaanza polepole, tukachukua 1,000 kwanza, eti Waziri wa Utumishi hatuwezi kuajiri hata 1,000? Hela si zipo kidogo, basi tuajiri madaktari 1,000, tuanze na 1,000, mambo yakiwa mazuri tena tutaongeza," aliagiza. Kuhusu maslahi na malimbikizo ya stahiki za watumishi wa sekta hiyo, Rais alisema wanaendelea kufanya uhakiki na kulipa madeni ya miaka ya nyuma na kwamba katika kipindi cha miaka minne, wamelipa Sh. bilioni 5.58. Alisema uhakiki unafanyika kutokana na kuwapo kwa watumishi hewa katika sekta mbalimbali na kwamba katika kipindi hicho waliwapandisha vyeo watumishi wa afya 7,804.

Alisema watumishi wa sekta ya afya ni 62,498 ambao mishahara yao katika kipindi cha miaka hiyo minne ni Sh. trilioni 4.169 wakati idadi ya watumishi wote serikalini ni 526,146, pasi na kuwajumuisha askari wa Jeshi la Wananchi (JWTZ). Alisema watumishi hao wa serikali wanalipwa Sh. bilioni 577 kila mwezi.

Kuhusu baadhi ya wanasiasa kuwanyanyasa madaktari na watumishi wengine wa sekta ya afya kwa kuwaweka ndani bila kufuata taratibu zilizowekwa kisheria, Rais alisema suala hilo haliungi mkono na tayari ameshawaonya viongozi katika vikao vya ndani.

"Ndiyo sababu watu hatukamatwi kamatwi, tumeshaambizana kwenye vikao vyetu vya ndani. Najua kiongozi akimkamata daktari na yeye siku akiumwa, akienda hospitali atamkamata," alitania.

Hata hivyo, zuio la kukamata na kuweka ndani madaktari na watumishi wengine wa kada ya afya, halitawahusu wanaokiuka maadili ya kazi na haki za binadamu kwa sababu suala hilo likiachwa, watu watakuwa wanafanya mambo ya ovyo.

Rais Magufuli pia aliitaka MAT kuwashughulikia watumishi hao wanaokiuka maadili ya utumishi kabla ya kushughulikiwa na wanasiasa.

## Barabara za kisasa kuing'arisha Kigoma

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amewahakikishia wananchi wa Kigoma na nchi za jirani kwamba serikali ipo kazini kupata fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara kuu ya ukanda huo kutoka Dar es Salaam.

Waziri Mpango aliyasema hayo jana mkoani Kigoma wakati wa hafla ya utiliaji saini mradi wa ujenzi wa barabara Manyovu-Kasulu yenye urefu wa kilometa 68.25.

Nyingine ni Kanyani Junction-Mbugwe kilometa 70.5, Mbugwe Nduta Junction-59.35, Nduta Junction-Kibondo Junction-Kabingo kilometa 62.5 ambapo jumla yake ni kilometa 260.6 zitakazogharimu zaidi ya Sh. bilioni 340.2.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Dk. Mpango aliwaeleza wananchi mkoani humo na nchi za jirani ambazo ni Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kuwa serikali inalishughulikia suala hilo ili kurahisisha ufanyaji wa biashara.

"Na hii ni pamoja na fedha za kulipa fidia kwa wananchi, tupo vizuri na fedha ipo, pia niwahakikishie wananchi wa Kigoma tulishapata fedha Dola za Marekani milioni 51 kutoka Kuwait Fund kujenga kipande cha barabara kutoka Chaya- Nyahua kilometa 85."

Dk. Mpango alimshukuru Rais John Magufuli kwa kuipaisha Kigoma kwa sababu iliyopo sasa siyo ile ya mwaka 2015. Kuhusu uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka huu, Dk. Mpango amewataka wananchi wachague viongozi na kutofanya makosa kwa kuwachagua wabinafsi.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Patrick Mfugale, alisema zabuni zilitangazwa kuanzia Machi mwaka jana na kampuni 167 ndizo zilichukua nyaraka ili wapatikane wanne.

Alisema waliorudisha zabuni ni 71 ndipo walipowapata hao wanne ambao walitia saini jana kwa ajili ya ujenzi wake utakaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 340.2.

"Makandarasi hawa wanatakiwa kuzijenga barabara hizi kwa muda wa miaka mitatu, tunaishukuru Benki ya Maendeleo Afrika (ADB) kwa kutoa hizo fedha na serikali kwa kutoa Sh. bilioni 58 ili kukamilisha mradi huu," alisema.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, aliwaeleza wananchi hao kuwa wabunge waliowachagua walikataa kupitisha bajeti ili kigoma iendelee kuwa ya mwisho, huku akiwaita mbele ambao walioipitisha.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema ujenzi wa barabara hiyo utawasaidia wanafunzi kwenda shuleni kwa raha na kuondoa adha kwa wananchi waliyokuwa wakiipata.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali mstaafu Emmanuel Maganga, aliwashukuru viongozi kwa kuigawa barabara hiyo sehemu nne ambapo itajengwa kwa wakati mmoja kwa vipande vyote.

# Majaliwa afunguka vitambulisho vya Taifa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema hatua ya serikali kuagiza umakini ufanyike katika utoaji wa vitambulisho vya Taifa hususani katika mikoa ya mipakani si kwa lengo la kutaka kumkomoa mtu, bali kuimarisha usalama wa nchi.

Aliyasema hayo jana baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wabunge wa Mkoa wa Kagera kuhusu usumbufu wanaoupata baadhi ya wananchi wanapofuatilia vitambulisho vya Taifa kwani wengine wanadaiwa kuwa si raia.

Malalamiko hayo yalitolewa wakati Waziri Mkuu akizungumza katika Mkutano wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Kagera. Waziri Mkuu ni mlezi wa CCM wa mkoa wa Kagera.

"Watu fuate taratibu katika suala la ugawaji wa vitambulisho, Idara ya Uhamiaji wafuatilie kwa umakini kwa sababu lazima usalama wa nchi usimamiwe ipasavyo hususani katika mikoa ya mipakani. Watanzania mnatakiwa muwe makini msiruhusu watu kuingia kwa njia za panya kwani watu hao hawana nia njema."

Waziri Mkuu alisema lazima zoezi hilo lifanyike vizuri na wataharakisha ili wananchi waweze kupata vitambulisho. Tayari serikali imeshaongeza vifaa na watumishi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ili waweze kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu amewataka viongozi na wanachama wa CCM waimarishe mshikamano miongoni mwao na pale kwenye dosari zirekebishwe kwa sababu hakuna jambo lisiloweza kutatuliwa.

"Tunahitaji kuwa na umoja na mshikamano ndani ya chama ili sote kwa pamoja tuweze kufikia malengo tuliyojiwekea...Hata katiba yetu ya chama inatuhimiza tushikamane kwani wote tunajenga nyumba moja hivyo hatuna sababu ya kugombea fito."

Waziri Mkuu alisema lazima wahakikishe kuwa CCM inabaki salama na kinaendelea kushika dola. "Ni wajibu wa kila kiongozi na mwanachama kuwezesha malengo hayo kutimia na ni lazima kila tawi litafakari namna ya kukiwezesha chama kujitegemea kiuchumi."

Pia Waziri Mkuu amewataka viongozi na wanachama wa CCM wajiepushe na suala la ukabila na udini katika kuteua mtu wa kugombea nafasi mbalimbali ndani ya chama hicho na badala yake wateue mtu ambaye anauzika ndani na nje ya chama.

## Hatima ya Lissu kukamatwa leo

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imepanga leo kusikiliza maombi ya wadhamini Ibrahim Ahmed na Robart Katula wa Mbunge wa zamani wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, kukamatwa.

Wawili hao wamefungua maombi mahakamani wakiiomba itoe hati ya kumkamata Lissu kwa kuwa wameshindwa kumpata.

Madai hayo yalitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, wakati kesi ya msingi ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba amri za awali kuhusu mshtakiwa Lissu zinaendelea na Upande wa Jamhuri unaomba wadhamini waieleze mahakama hatua walizofikia. Katula alidai wamefungua maombi mahakamani hapo kwamba wameshindwa kumpata Lissu na yamepangwa kutajwa leo mbele ya Hakimu Simba.

Wankyo alidai kuwa wamepokea nakala ya maombi ya wadhamini hao na kwamba wanasubiri leo kwa ajili ya kutajwa.

Mbali na Lissu washtakiwa wengine ni, Wahariri Simon Mkina, Jabir Idrisa na Mchapishaji wa Kampuni ya Jamana, Ismail Mehbooh.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao kwa pamoja, wanakabiliwa na mashtaka matano, likiwamo la kuandika habari za uchochezi kinyume cha Sheria ya Magazeti ya Mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari 12 hadi 14, 2016, jijini Dar es Salaam, washtakiwa Jabir, Mkina na Lissu, waliandika na kuchapisha taarifa za uchochezi zenye kichwa cha habari kisemacho, 'Machafuko yaja Zanzibar.'

Katika shtaka la pili, wanadaiwa kuwa Januari 14, 2016 walichapisha habari hizo ili kuleta chuki kwa wananchi wa Zanzibar. Mshtakiwa Mehboob anadaiwa kuwa Januari 13, 2016, katika jengo la Jamana lililoko Manispaa ya Ilala, alichapisha gazeti la Mawio lililokuwa na taarifa za uchochezi.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo pia alichapisha gazeti hilo bila ya kuwasilisha hati ya sheria ya kiapo kwa Msajili wa Magazeti.

# Wanafunzi 206 wapewa mimba

**Na Waandishi Wetu**

WANAFUNZI 11 kutoka shule saba za sekondari wilayani Liwale mkoani Lindi, wamekutwa na ujauzito katika kipindi kifupi cha kuanzia Januari hadi Februari mwaka huu.

Kati yao, wanne wanatoka Shule ya Sekondari Rashid Mfaume Kawawa, iliyopewa jina la aliyekuwa Waziri Mkuu enzi za uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Vilevile, imeelezwa kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari mwaka jana, wanafunzi 195 wa shule za msingi na sekondari wilayani Dodoma, wamepata ujauzito.

Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Sarah Chiwamba, aliiambia Nipashe jana kuwa wanafunzi hao wamebainika kufanyiwa ukatili huo baada ya kufanyiwa vipimo waliporejea shuleni kutoka likizo ya Desemba.

Mbali na Shule ya Sekondari Rashid Mfaume Kawawa, Chiwamba alizitaja sekondari zingine zilizokumbwa na baa hilo kuwa ni pamoja na Liwale Day ambayo wanafunzi wawili wamegundulika kuwa na mimba, Barikiwa (wawili) na Mihumo (mmoja).

"Sekondari zingine ni Kiangara (mmoja) na Kibutuka (mmoja)... upimaji unaendelea na kufikia wiki ijayo, kazi hiyo itakuwa imemalizika kwa sekondari zote 17 za wilaya yetu ya Liwale," alisema.

Chiwamba alisema wana utaratibu wa kuwapima wasichana kila wanapotoka likizo na ndiyo maana hao wamegundulika, akieleza kuwa upimaji ulianza mara tu baada ya shule kufunguliwa.

"Mimba hizo wametoka nazo nyumbani kwao walipokuwa likizo, lakini jitihada zinaendelea za kukabiliana na tatizo hili kwa kuanzisha klabu za kutokomeza mimba na ukatili wa kijinsia," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alisema hatua hiyo inaambatana na kutoa elimu ya uzazi na masuala mengine kwa ajili ya kumsaidia mtoto wa kike kujiamini kama njia mojawapo ya kumaliza tatizo hilo.

Alikumbusha tukio la mimba lililowahi kutokea wilayani mwake na kumsikitisha la mwanafunzi wa kidato cha pili aliyejifungua akiwa shuleni wakati anaendelea na mitihani.

Alisema mwanafunzi huyo alikuwa akiishi bwenini na alikutwa na tukio hilo akiwa katika mazingira ya shuleni, usiku wa kuamkia Novemba 15 mwaka jana.

"Wito wangu ni kwamba wazazi kuendelea kushirikiana kutokomeza mimba za utotoni kwa ajili ya maendeleo ya elimu ya mtoto wa kike, waungane nasi katika juhudi za kutoa elimu ya uzazi na mambo mengine muhimu," alishauri.

Mimba kwa wanafunzi ni miongoni mwa matatizo yanayousumbua Mkoa wa Lindi. Mkuu wa Mkoa huo, Godfrey Zambi, alisema kulikuwa na mimba 151 kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika mkoa huo kwa miezi tisa ya mwanzo wa mwaka jana.

**MIEZI 12 MIMBA 195**

Wakati hali ikiwa hivyo Liwale, wilayani Dodoma imeelezwa kuwa katika kipindi cha miezi 12 iliyoanzia Januari mwaka jana hadi Januari mwaka huu, wanafunzi 195 wa shule za msingi na sekondari wameripotiwa kuwa na mimba.

Kutokana na baa hilo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Patrobas Katambi, ametangaza kuanza upelelezi wa kina ili kuhakikisha hatua zinachukuliwa kwa waliowapa mimba wanafunzi baada ya kubaini kuwapo kwa tatizo la kesi za aina hiyo kuvurugwa.

Alibainisha kuwa kati ya matukio hayo, nane yanawahusu wasichana wa shule za msingi.

"Kesi hizi kuna urasimu, rushwa na uvunjaji wa sheria na taratibu kwa sababu hakuna kifungo wala shauri mahakamani linaloendelea.

"Kesi zinaharibiwa kwa hila na kuharibu maisha ya watoto wangu wa shule na kuingiza umaskini katika familia na jamii, naanza upelelezi wa kina mwenyewe tuone haki ikitendeka.


CONTRACTORS REGISTRATION BOARD

Contractors Training Course

Bukoba , February 24 - 26, 2020

Construction Pre- Contract Practice

*ELCT Hotel – Bukoba*

The Contractors Registration Board wishes to inform all Contractors that a special training course on **Construction Pre- Contract Practices (Module SC 120/ MC 220)** will take place in **Bukoba** at the ELCT Hotel starting at **8:30 on Monday 24th to Wednesday 26th February 2020**

The course is highly interactive and practice-oriented and will cover project procurement systems; the role of the contractor; bidding strategies; risk management; tendering procedures; construction cost estimating; construction methods and preparation of method statements; modern planning tools; resources forecasting and negotiations.

The course is targeted at Managing Directors (MDs), Directors, Architects, Engineers, Quantity Surveyors and Technicians from Firms registered with CRB and Technical personnel from other Institution dealing with Construction.

The fees for the course is **50,000/=** per person for Registered Contractors and **100,000/=** for non contractors.

The Fees covers training materials, lunch and beverages for three days. Fees are to be paid directly to Bank of Tanzania, CRDB, NBC, and NMB in the name of **CONTRACTORS REGISTRATION BOARD** using control number **995740012554**

**The Board wishes to inform Contractors and other construction industry practitioners of other upcoming courses under the SSTP Programme in Year 2020 as follows:-**

| Center | Date | Course |
|---|---|---|
| *Njombe* | 25-27/03/2020 | Business Management Skills |
| *Morogoro* | 06-08/05/2020 | Procurement of Works |
| *Dodoma* | 03- 05/06/2020 | Construction Pre- Contract Practice |

***For further inquiries, please contact:***

*Contractors Registration Board, 3rd Fl., Tetex Hse, Pamba Road, P. O. Box 13374, **DSM***
*Tel No: 2131169/ 2137962-3, Fax No: 2137964, E-mail: crbhq@crbtz.org; Web-site: www.crb.go.tz*

*or*

*Contractors Registration Board, East Zone Office, Coca cola road Mwenge, Josam Hse 4th Floor, P. O. Box 33621, **DSM***
*Tel +2552771877, E-mail: crbez@crbtz.org;*

*or*

*Contractors Registration Board, Lake Zone Office, **TANROADS** Compound, P. O. Box 2815, **MWANZA***
*Tel No: 028-2500218, E-mail: crblz@crbtz.org;*

*or*

*Contractors Registration Board, Southern Zone Office, **NHIF TOWER,3rd** Floor, P. O. Box 1690, **MBEYA***
*Tel No: 025-2502480, Fax No: 025-2502580, E-mail: crbsz@crbtz.org;*

*or*

*Contractors Registration Board, Northern Zone Office, 4th Floor Block B Summit Centre, P. O. Box 16795, **ARUSHA***
*Tel/ Fax No: 027-2547107; E-mail: crbnz@crbtz.org;*

*or*

*Contractors Registration Board, Central Zone Office, 1st Floor PSPF Plaza, P. O. Box 2618 **DODOMA***
*Tel/ Fax No: 0262966040/262966041*

**REGISTRAR**

215639102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viongozi chungeni ndimi kulinda amani

**MWENYEKITI** wa NCCR - Mageuzi James Mbatia, katika hotuba yake ya ufunguzi wa moja ya mikutano ya chama chake, anakumbusha umuhimu wa kuchunga ulimi katika kipindi hiki taifa linapoelekea kwenye uchaguzi mkuu.

Joto la uchaguzi linaendelea kupanda kwa vile Oktoba mwaka huu ndiyo wakati wa kuchagua wabunge, madiwani na rais kwa upande wa Tanzania Bara.

Kwa upande wa Zanzibar wanamchagua Rais wa Zanzibar, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wabunge wa kuwawakilisha bungeni.

Tunaungana na msimamo wa wapenda amani na ustawi wa taifa, kama Mbatia ambaye anashauri kuwa ni wakati wa kulinda ulimi na kuchunga kauli zetu.

Hata, pale tunapozungumza hasa kauli za kisiasa ni wakati wa kuiweka Tanzania mbele kwa kila kitu tunapokitaja hasa kipindi hiki tunapoingia kwenye mchakato na maandalizi ya uchaguzi mkuu.

Kila linalotamkwa kwa vinywa vyetu hasa viongozi lihakikishe kuwa linanena mema kwa ajili ya taifa, linalinda amani, maridhiano, uzalendo, umoja na mshikamano.

Ifahamike kuwa kwa maneno upo uwezekano wa kuvunja umoja wa Watanzania na pia kwa kauli zetu viongozi tunaweza kusababisha anguko kwenye taifa letu.

Tungependa kukumbushana kuwa ni wakati wa kuongeza uvumulivu wa kisiasa. Wapinzani wana kila sababu ya kuwa wavumilivu dhidi ya chama na serikali iliyoko madarakani.

Lakini ni muhimu serikali na chama kinachoongoza kuvumilia upinzani ili kuwa na demokrasia inayohimiza kuvumiliana iwe kisiasa, kidini, kikabila na hata kikanda.

Ikumbukwe kuwa wakati tunapoelekea kwenye uchaguzi ni muda ambao kila mmoja angependa kusema kila anachoona kinafaa kusikika na kuongelewa na wananchi ili kujipatia tija na kuwa na manufaa zaidi kisiasa.

Halikadhaliki ikumbukwe kuwa wapo wasiokubaliana na fikra zake na hoja zake ambao nao hawatakaa kimya ni lazima watampinga. Tunaomba kueleza kuwa tunaposema kuchunga ndimi tunamaanisha kwa kila mdau kuanzia, wanasiasa, viongozi wa dini, wazee wa mila, asasi za kiraia na vyombo vya mawasiliano.

Wote tunawajibika kulinda kauli zetu kwa sababu tuna ushawishi na uwezo wa kufikisha ujumbe unaoweza kusababisha uvunjifu wa amani na hata chuki za kisiasa.

Kwa upande mwingine, hizi ni zama za kidijitali ambazo zinaruhusu kutumia mitandao ya mawasiliano kutoa kauli nyingi za kuchafuana na hata kuharibiana kisiasa, kijamii na hata kifamilia.


Yote hayo ni mambo ya kuepuka kwa sababu wote ni Watanzania na kikubwa tunachotakiwa kukitetea ni taifa letu na wala si kuwasifia au kuwatukana marafiki au maadui zetu wa kisiasa, kiimani au kikabila.

Tunasisitiza kuwa kuna umuhimu wa kujilinda na kujiepusha na kauli na maandiko yanayovuruga amani na mshikamano wa taifa. Wenye mamlaka wazungumze ukweli na kuiarifu jamii mambo ya msingi ambayo yatawawezesha wananchi kupendana na kuheshimiana. Mambo ambayo yatawaleta pamoja raia ili washindane kwa hoja badala ya kuwatenganisha na kuongeza uadui kupitia matamshi ya majukwaani na kwenye mitandaoni.

Lakini ni wakati wa kushindana kwa hoja na mikakati badala ya matusi na kauli za kuudhi zinazosababisha kuchochea hasira, chuki na wivu. Tunawakumbusha viongozi wanaohama vyama si wakati wa kukichafua chama ulichokuwa unakitumikia.

Ni vyema kuchunga ulimi ili kuweka ushindani wa hoja na mikakati majukwaani badala ya matusi, kejeli na kauli za kuudhi zenye kutishia amani na uvumilivu wa kisiasa miongoni mwa wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kulikoni biashara ya mifuko plastiki nchini?

Na Sabato Kasika

**MIFUKO** ya plastiki ilipata umaarufu mkubwa nchini, kutokana na unafuu wa bei yake, hali ambayo ilisababisha watu wengi kupenda kutumia kubebea bidhaa mbalimbali madukani na sokoni.

Kulikuwapo kundi kubwa la vijana waliokuwa wafanyabiashara wa mifuko hiyo, iliyopatikana kwa wingi karibu maeneo yote ya mijini; sokoni, madukani na wapo wauzaji walioufuata, huku baadhi yao wakitafutia wateja mitaani.

Hata hivyo, Juni Mosi mwaka jana, serikali ilipiga marufuku matumizi ya mifuko ya mifuko hiyo, ikiwa tayari imeandaa mbadala wake, kwa lengo la kulinda na kutunza mazingira.

Tangu wakati huo mifuko mbadala inayotengenezwa nchini, ndiyo imekuwa ikitumiwa na Watanzania kwa kubeba vitu mbalimbali na hasa wanapokwenda kununua mahitaji dukani au sokoni.

Wakati mifuko hiyo inayotengenezwa nchini, ikiendelea kutumiwa na wananchi, imebainishwa kuwa kuna mifuko ya plastiki inayoingizwa sokoni kinyemela, kutoka nchi za jirani na kuanza kutumiwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Zungu, anaonya wananchi kuchukuliwa hatua kwa kuhujumu uchumi.

Zungu anasema, mifuko hiyo siyo salama wala imara anawataka Watanzania kuipenda mifuko ya kwao ya asili, kuchangia kodi kwa ajili ya maendeleo yao. Anasema, wamebaini mifuko ya plastiki, imeshaanza kurudi na msisitizo wake ni kwamba wananchi waiache, badala yake wajikite kutumia mbadala wake, ambayo inatengenezwa na viwanda vya chini.

Kutokana na maelezo ya waziri, ni kwamba kuna haja ya kuziba njia zote za panya ambazo zinatumika kuingiza bidhaa kinyemela ili kulinda bidhaa za hapa nchini pamoja na afya za Watanzania.

Bidhaa ambazo zimepigwa marufuku nchini, haziwezi kuingizwa kihalali, badala yake wahusika watatumia njia za panya, ambazo wanaamini kwamba hakuna mtu wa kuwakagua.

Hivyo, waziri aweke mtego kila eneo ambalo anadhani kwamba linaweza kuwa ni uchochoro wa kupitishia bidhaa au biashara isiyofaa na kuingizwa nchini, ili iwe rahisi kuwanasa wahusika na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Watanzania nao kwa upande wao wanatakiwa kushiriki katika vita hii ya biashara kwa kuwafichua wahusika wa uhalifu huu ili kuhakikisha mifuko inayotengezwa nchini inaendelea kupata soko.

Inashangaza kusikia mifuko ya plastiki imeanza kuingizwa kutoka nchi jirani na kuuzwa sokoni kana kwamba hakuna marufuku, wanaofanya hivyo wanataka kuirudisha nyuma Tanzania.

Inawezekana mifuko hiyo imepata soko kutokana na Watanzania wenyewe kuichangamkia, labda kwa unafuu wa bei, ila bado watambue ni hatari, hivyo wasiangalie unafuu tu bali usalama wa afya zao.

Serikali iliondoa biashara ya mifuko hiyo sokoni na kuleta mbadala wake, kutokana na ukweli kwamba ina madhara, sasa wanapojitokeza baadhi ya watu na kuiingiza kinyemela, hawatakii mema Watanzania.

Biashara ya mifuko ya plastiki inapigwa vita katika nchi mbalimbali duniani ingawa ina fursa za kiuchumi kutokana na watu wengi kuiuza, lakini inalazimu kuachana nayo kutokana na madhara yake.

Kimsingi, wataalamu wa mazingira wanasema, mifuko mingi ya plastiki haiozi hata inapofukiwa ardhini na kuifanya ardhi ikose rutuba na wakati mwingine, inasababisha ardhi hiyo isifae kwa kilimo.

Aidha, mifuko hiyo inaweza kuanza kuoza baada ya miaka 20 au zaidi na kwamba, hata wanyama kama ng'ombe, kondoo, mbuzi na wengine wa aina hiyo wanaweza kufa wanapokula mifuko hiyo.

Wanyama hao wanaweza kula kutokana na ukweli kwamba wapo watu wanaoitupa ikiwa na mabaki ya chakula, hivyo wanaweza kuimeza pamoja na hicho chakula na mwisho wa siku wakafa.

Kikubwa, Watanzania walioachana na mifuko hiyo, wasikubali kurudishwa nyuma na wachache wanaotaka kujinufaisha, bali waendelee kutumia mbadala, katika ambavyo serikali inaelekeza.

Ni muhimu kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa nchini ni zile zinazotakiwa kwa manufaa ya afya za Watanzania, pia kulinda na kutunza mazingira. Hivyo ni vyema kuwafichua wahusika, ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Tukumbuke onyo la waziri, hivyo wanaoingiza mifuko na wanaootumia, watambue kuwa wanajiweka katika mazingira ya kwenye hatia. Watafakari, kisha wachukue hatua za kuachana na biashara hiyo.

# Taasisi elimu kwa vijana yapewa ruzuku

**Na Friday Simbaya,** MBEYA

TAASISI isiyokuwa ya kiserikali ijulikanayo kama elimu kwa vijana kupitia michezo (YES TZ), imepokea msaada wa ruzuku ya Dola za Marekani 42,000 (sawa na Sh. 97,012,986.775), kwa ajili ya matumizi ya kuijengea taasisi uwezo.

Kwa kufanya hivyo, itatekeleza majukumu yake ya kusaidia serikali kufikia malengo mbalimbali.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Kenneth Simbaya, alisema ruzuku hiyo imetolewa kutoka Open Society Initiative for Eastern Africa (OSIEA), na kwamba fedha hizo zitatumika kuanzia Januari 2020 mpaka Juni 30, 2021.

Alisema kupitia waelimishaji rika wa kujitolea wa taasisi hiyo, kumekuwa na ongezeko kubwa la vijana ambao wamepata mafunzo toka kwa vijana wenzao wanaojitolea.

Aidha, Simbaya alisema waelimishaji rika hao wamepeleka elimu sahihi kwa vijana wenzao ambayo imekuwa msaada mkubwa.

Alisema vijana 4,000 walifikiwa na vijana wa kujitolea na wengi wao ni wanawake kutoka kata tisa.

Mwelimishaji rika wa kujitolea, Katie Dunbar, alisema kujitolea kuna faida kubwa sana kwa vijana kwani wanajifunza vitu vingi na kupata uzoefu wa kufanya kazi.

"Mfano mimi mwenyewe hapa nimejifunza vitu vingi kwa kujitolea, ukiachilia mbali kupata uzoefu wa kujitolea kufanya kazi kumeniwezesha kukuza mtandao wa watu ninaowafahamu ambao ni muhimu katika maisha yangu ya kikazi pamoja na kuongeza marafiki," alisema Dunbar.

**Kupitia waelimishaji rika wa kujitolea wa taasisi hiyo, kumekuwa na ongezeko kubwa la vijana ambao wamepata mafunzo toka kwa vijana wenzao wanaojitolea.**

# Walalamikia eneo la fukwe kuharibu maadili ya watoto

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANANCHI wa Konde Wilaya ya Micheweni Pemba wameiomba serikali kuweka mikakati madhubuti kwa watu wanaoingia katika fukwe ya Vumawimbi Makangale, ili kulinda maadili na heshima ya wanajamii wa maeneo hayo.

Wananchi hao walisema watu wanaoingia kutembea katika fukwe hiyo hawana maadili mazuri, jambo ambalo linasababisha watoto wao kuiga mambo yasiyofaa.

Walisema ipo haja kwa Serikali ya Wilaya ya Micheweni kuweka mikakati madhubuti kwa watakaoingia katika eneo hilo, ili kufuata mila, silka, tamaduni na maadili mema, ambayo yatasaidia kuendeleza heshima kwa wakazi wa maeneo yaliyokaribu na fukwe hiyo.

"Kwa kweli sasa tuna shaka kubwa, watoto wetu wanaiga kila wanachokiona, maana watu wanaoingia Vumawimbi ni mtihani tu tofauti na zamani, hawana heshima wala maadili," alisema.

Hindu Hamad Bakar, alisema heshima ya fukwe ya Vumawimbi imetoweka kutokana na watu wanaoingia kufanya mambo kinyume cha maadili yao, jambo ambalo linawakera sana.

"Wanatoka nyumbani kwao wamevaa vizuri, wanapofika huku wanavua nguo na kubaki wanavyotaka wenyewe, tena wanaokuja ni watoto kati ya miaka 15 na 16 akiwamo wanaume na wanawake, ambao huchukuliwa na wanaume watu wazima," alisema.

Mchanga Said Seif, alieleza kutokuwa na usimamizi madhubuti katika fukwe hiyo kunasababisha watoto wanaofikishwa hapo kufanyiwa vitendo vya ulawiti na ubakaji.

"Wanapofanya vitendo hivi na watoto wetu huiga na ndio maana muda wote wanakwenda Vumawimbi, hivyo ni mtihani, tunahitaji msaada," alisema.

Naye Kiongozi wa dini, Omar Khamis Hamad, alieleza kuwa watoto wanaokwenda kwenye fukwe ya Vumawimbi wanadhalilishwa kupita kiasi.

Aliiomba serikali isiangalie mapato tu bali waangalie na maadili ili kuwalinda watoto na kulinda heshima ya wananchi wa maeneo yaliyokaribu na fukwe.

Sheha wa Shehia ya Konde, Mohamed Omar Abdallah, alisema, fukwe ya Vumawimbi ni chanzo cha mapato ingawa wanaoingia wanaharibu maadili.

"Serikali ipange mkakati na kuweka utalii salama, hii itasaidia kuingiza kipato kwa watalii wa ndani na nje, pia italinda maadili yetu mila na tamaduni," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Micheweni, Salama Mbarouk Khatib, alieleza kuwa waliweza kudhibiti eneo hilo na watoto walikuwa wanakwenda na wazazi wao.

" Wazazi waendelee kwenda pamoja na watoto wao, waone kuwa si eneo rafiki kwa watoto peke yao, hivyo watakapokuwa pamoja wataepuka kufanyiwa udhalilishaji," alisema.

Fukwe ya Vumawimbi ni sehemu ya utalii wa ndani ambayo hutumiwa na wananchi kisiwani Pemba, ingawa wakazi wa maeneo hayo wanachoshwa na tabia zinazofanywa na watu wanaofika hapo.



Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Wilson Mahera, akizungumza na wanahabari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuongeza muda wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kushoto ni Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Elimu ya Mpigakura, Giveness Aswile. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kibaha yatekeleza miradi mikubwa mitatu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

HALMASHAURI ya Mji wa Kibaha mkoani Pwani, iko katika utekelezaji wa miradi mikubwa mitatu, ambayo ni hospitali ya wilaya, machinjio, soko la kisasa na jengo la halmashauri.

Hayo yamebainishwa na Ofisa Uhusiano wa Halmashauri hiyo, Innocent Byarugaba, katika mahojiano na Nipashe.

Byarugaba alisema, miradi hiyo ikikamilika itaondoa changamoto zilizokuwapo awali, lakini maendeleo katika mji huo yatapatikana ikiwamo kukuza kipato kwa wananchi na ongezeko la makusanyo ya mapato ya ndani.

Akizungumzia ujenzi wa hospitali ya wilaya katika halmashauri ya mji, alisema, utasaidia kuondoa msongamano katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Tumbi.

Alisema, katika mwaka wa fedha 2018/2019, halmashauri hiyo ilitumia Sh. 1,790,000 kwa ajili ya majengo mbalimbali ya hospitali hiyo, ambapo Sh. bilioni 1.5 ni fedha kutoka Serikali Kuu na Sh. 290,000,000 ni mchango kutoka halmashauri hiyo.

Byarugaba alisema, majengo saba yamejengwa katika hospitali hiyo na kwa sasa yapo katika hatua za utekelezaji likiwamo jengo la wagonjwa, mama na watoto, mionzi, maabara, utawala na jengo la stoo ya dawa na la kupokea umeme.

Aidha, alibainisha kuwa, katika mradi wa soko la kisasa unatarajia kugharimu Sh. bilioni nane, unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu.

Byarugaba alisema kukamilika kwa soko hilo la kisasa itaondoa changamoto ya wakazi wa Mji wa Kibaha na maeneo ya jirani kufuata bidhaa katika Soko la Kariakoo.

Alisema, mradi wa machinjio kwa sasa unaendelea kutekelezwa katika awamu ya pili na upande wa jengo la ofisi ya halmashauri kwa sasa iko katika awamu ya nne baada ya kukamilika kwa awamu kwanza hadi ya tatu ambayo ilianza mwaka 2011/2012 , Sh. 7,065,111,496 hadi kukamilika.

# Waziri anusa ufisadi mradi wa maji

**Na Dege Masoli,** MKINGA

NAIBU ya Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ameagiza kuchunguzwa ujenzi wa mradi wa chanzo cha Maji cha Mbuta katika kata Mwakijembe wilayani Mkinga kwa kile alichobaini kuwapo kwa ufisadi wa zaidi ya Sh. milioni 400 ambazo licha ya kutumika lakini hakuna kazi iliyofanyika.

Aweso alitoa agizo hilo juzi alipokuwa kwenye ziara ya siku moja wilayani hapa kutembelea miradi ya maji.

Baada ya kufika kwenye mradi wa maji wa Mbuta unaotekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.7, hakuridhishwa na matumizi ya Sh. milioni 400 zilizodaiwa kutumika kuchimba bwawa.

Kutokana na kutilia wasiwasi matumizi ya fedha hizo, aliagiza kuundwa timu ya uchunguzi wa matumizi ya fedha hizo akiwamo mkandarasi wa mradi, Kampuni ya White City pamoja na kamati iliyohusika kwenye utekelezaji huo.

Pia aliagiza kukamatwa kwa msimamizi wa mradi huo, Mhandisi Castory Kenneth, kwa kile alichodai kutokuwa makini kusimamia wajibu wake na kusababisha matumizi mabaya ya fedha za serikali.

Naibu Waziri pia alihoji ulazima wa watekelezaji wa mradi huo kuanza kujenga matangi na kusambaza mabomba badala ya kushughulikia chanzo cha maji kwanza jambo alilodai ni kukosa uadilifu na kutaka kupata asilimia 10.

"Hawa mabwana najua walikimbilia kusambaza mabomba na kujenga matangi kwa kuwa huko ndipo kwenye asilimia 10 ya haraka, vinginevyo wangeelekeza nguvu kutengeneza chanzo kabla ya kazi waliyoifanya," alisema Aweso.

Hata hivyo, Aweso alipongeza mradi wa maji wa Mwakijembe kutokana na kile alichokieleza mwonekano unaolingana na thamani ya fedha baada ya kuelezwa kuwa ujenzi wa chanzo hicho umegharimu zaidi ya Sh. milioni 200 huku matumaini ya kazi hiyo yakionekana.

Akizungumza katika majumuisho ya ziara hiyo, Aweso aliwataka wataalamu kubadilika na kutumia elimu yao kwa faida ya wananchi na taifa kwa ujumla na kwamba utendaji kazi wa ujanjaujanja hautawasaidia.

Alisema wataalamu ndio tegemeo kubwa la serikali na kwamba wasitumie ugumu wa mazingira ikiwamo miundombinu kama sehemu ya kula fedha za miradi zinazotolewa na serikali au wafadhili kwa kuwa hawatakuwa salama kwa kufanya hivyo.

Naibu Waziri alisema wananchi wana matatizo mbalimbali ya ukosefu wa maji na wanataka huduma hiyo huku akisisitiza kuwa serikali imekusudia kuwaondolea changamoto hiyo wananchi, hivyo wataalamu wasiwe vikwazo.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (kulia), akizungumza na Kaimu Balozi wa Marekani nchini, Dk. Imni Patterson, kuhusu masuala mbalimbali ya ushirikiano kati ya nchi yake na Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WMNN**

# Wanawake wapewa mbinu za kushika uongozi wa juu

**Na Gwamaka Alipipi**

CHAMA cha Waajiri Tanzania (ATE) kimezindua awamu ya tano na sita ya mafunzo ya kuwajengea na kuwaandaa wanawake kushika nafasi za juu za uongozi.

Mafunzo hayo ya miezi tisa yamehudhuriwa na wanawake 44 kutoka taasisi mbalimbali za binafsi na serikali.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa ATE, Dk. Aggrey Mlimuka, alisema mafunzo hayo yatawajengea uwezo wanawake namna ya kujieleza, kusimama na kutetea jambo mbele ya umati wa watu bila woga pindi wanaposhika nafasi za juu katika bodi.

Dk. Mlimuka alisema mafunzo hayo pia yatawawezesha wanawake kuwa na mchango katika kampuni zao na nchi kwa ujumla. "Washiriki wametoka mikoa mbalimbali, ni kozi ya miezi tisa lakini wanakaa darasani kwa siku 14 tu, muda wao mwingine wa mafunzo watautumia wakiwa kazini.

"Tunawaandaa katika mambo matatu: Kwanza; wawe viongozi katika kampuni na taasisi zao. Pili; wawe wajumbe wa bodi za wakurugenzi na tatu; tunawafundisha namna ya kuandaa hotuba nzuri, weweze kuwa na ujasiri wa kusimama mbele ya watu, pia tunataka wawe wazungumzaji wazuri," alitamba.

Aliongeza kuwa dhumuni lingine la mafunzo hayo ni kuwaandaa wanawake kushika hatamu katika nafasi za uongozi pamoja na kuwa wakurugenzi wa mashirika ya bodi.

"Tulianza kutoa mafunzo haya mwaka 2016 na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan ndiye aliyefungua mafunzo ya kwanza, kila mwaka tumekuwa na kozi moja, lakini mwaka huu tumekuwa na kozi mbili na tutawagawa wanawake katika makundi mawili," alisema.

Profesa Bonard Mwape kutoka Chuo Kikuu cha Uongozi Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAMI), mmoja wa wawezeshaji wa mafunzo, alisema mafunzo hayo yatawasaidia wanawake kujielewa, kujiamini na kuwa na uwezo wa kuongoza.

Alisema wanawake wengi wanakuwa na woga wa kuamua jambo ama kutoa uamuzi kwa kuhofia kuchekwa ama kudharauliwa.

Profesa Mwape alisema ushiriki wa wanawake katika nafasi za juu za uongozi huongeza chachu ya ufanyaji kazi na uzalishaji katika sehemu wanazozisimamia.

## DC aonya wafanyabiashara kushindwa kutoa risiti EFD

**Na Steven William,** MUHEZA

MKUU wa Wilaya ya Muheza, Mhandisi Mwanasha Tumbo, ameagiza wafanyabiashara wilayani hapa, wanaomiliki maduka ya vyakula, kutoa risiti pindi wanauza bidhaa hizo ili serikali ipate mapato.

Agizo hilo alilitoa juzi katika semina ya mafunzo ya siku moja kwa wafanyabiashara na wasafirishaji iliyofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Muheza, mjini hapa.

Tumbo alisema wafanyabiashara katika Wilaya ya Muheza ambao wananunua bidhaa mbalimbali wanatakiwa wadai risiti na wakati wa kuuza watoe risiti ili serikali ipate fedha kupitia kodi kwa ajili ya kuendeleza huduma za kijamii.

Alisema kununua bidhaa bila kupewa risiti ni kosa kwa kuwa mtu anaweza kuuziwa mzigo wa magendo au bidhaa za vyakula zikawa hazina viwango na kuhatarisha usalama wa watumiaji.

Tumbo alisema wafanyabiashara lazima walipe kodi kwa kuwa wasipolipa kodi kutakuwa hakuna maendeleo huku akiitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikadirie kiwango halali ili wafanyabiashara walipe kodi kwa moyo.

Katika kutekeleza hilo, Tumbo alisema atawasiliana na Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD) ya Muheza, Cosmas Maziwa, kuanza msako dhidi ya wafanyabiashara ambao wanauza bidhaa, lakini hatoi risiti ili wachukuliwe hatua.

Alisema lazima TRA ikusanye kodi kwa wingi kwa wafanyabiashara ili serikali iweke miundombinu bora na kwa sasa serikali imeingia mkataba na mkandarasi wanajenga barabara kutoka Muheza Mjini kwenda Tarafa ya Amani kilomita 40 na kusaidia ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya ambayo serikali imetoa Sh. bilioni mbili.

Mfanyabiashara na msafirishaji wilayani Muheza, Salimu Acha, alisema wanalipa kodi lakini serikali haitengenezi barabara ya kutoka Muheza mjini kwenda Amani, hatua ambayo inasababisha magari yao ya kusafirisha abiria kuharibika.

Juma Semauto, mfanyabiashara anayeuza vyakula ikiwamo unga maeneo ya mashine nyingi, alisema kuwa wafanyabiashara wengi hawana elimu ya kulipa kodi, hivyo huduma hiyo inahitajika sana kwao.

Mfanyabiashara wa kusafirisha mizigo, Saidi Seif, alisema wana changamoto kubwa katika biashara yao ya malori wakipakia mizigo lakini wamekuwa wakikadiliwa kodi kubwa ya mapato katika vizuizi vya ukaguzi vya TRA.

# TPA yafunga mitambo bora chuoni kwake

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imekamilisha ufungaji wa mitambo miwili ya kisasa katika Chuo cha Bandari jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya kufundisha kwa vitendo.

Mitambo hiyo ambayo imeanza kutumika kutoa mafunzo kwa vitendo, inatarajiwa kutatua tatizo lililowakumba wanafunzi kufanya mafunzo kwa vitendo baada ya kukamilisha mafunzo ya nadharia.

Akizungumza baada ya kuzindua mitambo hiyo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, alisema usimikwaji wa mitambo hiyo ni hatua kubwa iliyofikiwa na TPA na serikali.

Alisema lengo ni kuhakikisha Chuo cha Bandari kinafanya mabadiliko na maboresho katika utoaji wa taaluma ya shughuli za bandari kwa weledi mkubwa na kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia.

"Serikali inafuatilia kwa karibu utendaji na maendeleo ya taasisi zake mbalimbali ikiwa ni pamoja na Chuo cha Bandari, tunazo taarifa kuhusiana na juhudi zinazoendelea za kuboresha chuo hiki hii ni pamoja na kufahamu kwamba tayari mmepata ithibati kamili baada ya kuikosa kwa muda mrefu," alisema.

Nditiye alisema ni vyema chuo kikikamilisha mapema kazi ya kupitia upya mitaala yake kwa kuwa iliyopo inahitaji kuhuishwa sambamba na kuandaa mitaala mipya ili kukidhi mahitaji ya sasa ya soko la ajira hususan itakayokidhi mahitaji ya serikali ya kuinua uchumi wa viwanda.

"Nakuhimiza Mkuu wa Chuo kuendelea kutekeleza miongozo na maelekezo ya Bodi ya Wakurugenzi ya TPA ipasavyo na serikali itaendelea kufuatilia utendaji na maboresho ya chuo ili lengo la kufikia ufanisi wa utendaji wa wanafunzi wanaohitimu katika chuo hiki litimie," alisisitiza Nditiye.

Aidha, alisema wizara inazo taarifa kuwa Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya TPA ipo katika mazungumzo na Chuo cha Utalii pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la miundombinu.

Nditiye aliagiza kazi hiyo ikamilike kwa wakati uliopangwa bila kuwapo kwa ucheleweshaji.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo na Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Deusdedit Kakoko, aliiomba serikali kusaidia kukamilisha urejeshwaji wa miundombinu na majengo hayo ili kukiwezesha chuo kufundisha vijana wengi zaidi.

"Bodi ya Chuo ilipokea taarifa ya utendaji na kubaini kuwa kuna upungufu mkubwa katika eneo la miundombinu hususani madarasa, ofisi za wakufunzi na maofisa utawala wa chuo hali hii imetokana na uamuzi wa serikali uliofanywa mwaka 2001 wa kugawa sehemu kubwa ya majengo ya Chuo cha Bandari kwenda chuo cha hoteli na utalii ambacho kimeshajenga jengo lake," alisema.

Naye Mkuu wa Chuo cha Bandari, Dk. Joseph Kakeneno, alisema chuo kina jumla ya wanafunzi 532 na inatarajiwa kwamba udahili wa Machi 2020 utaongeza idadi ya wanafunzi kufikia zaidi ya 800.

# Watoto wenye ualbino wapata msaada

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATOTO wenye ualbino wanaolelewa kwenye kituo cha Buhanghija Jumuishi Shinyanga Mjini, wamepewa msaada wa vitu mbalimbali na chakula.

Akizungumza wakati wa kutoa msaada huo jana, Mkurugenzi wa Kampuni ya Jambo, Esme Salum, alisema wameamua kutoa sehemu ya faida wanayoipata, kusaidia watoto hao wenye ualbino ili kuwapa faraja.

Alisema watoto wenye ualbino wanapaswa kutembelewa na kupewa misaada ya vitu mbalimbali ikiwamo chakula, ili wapate kufarijika na kujiona jamii ipo pamoja nao.

"Sisi kampuni ya Jambo tumeambatana na wachezaji wa timu ya Stand United ya hapa Shinyanga Mjini ambayo tunaifadhili, kuja kutoa msaada wa vitu mbalimbali kwa watoto hawa wenye ualbino, ikiwamo unga wa ngano, chumvi, sabuni za kufulia, mafuta ya kujipata pamoja na juice," alisema Salum.

"Utoaji msaada utakuwa endelevu kwa sababu bado wanahitaji msaada wetu wa kutatua baadhi ya changamoto ambazo zinawakabili ili wapate kuishi kwa furaha," aliongeza.

Nao baadhi ya watoto hao akiwamo Simon Paulo, wameishukuru kampuni hiyo kwa kutoa msaada huo na kuwaomba wadau wengine wa maendeleo wajitokeze kuwasaidia.

Msimamizi mkuu wa kituo hicho, Mwalimu Selemani Kipanya, alisema wanafarijika kwa msaada huo na kutaja watoto wanaohifadhiwa kwenye kituo hicho kuwa ni 228, wasioona 23, ulemavu wa usikivu 74 na wenye ualbino 131.

# Tabora yapata bil. 8/- ujenzi hospitali, vituo afya

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 8.8 kwa Mkoa wa Tabora kwa ajili ya kukarabati na kujenga hospitali na vituo vya afya katika kipindi cha 2015 hadi Desemba 2019 ili kusogeza huduma za utoaji wa tiba kwa wananchi.

Hatua hiyo imeondoa adha kwa wananchi kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya na kurahisisha upatikanaji wa vifaa tiba na huduma za upasuaji katika maeneo yaliyo karibu na wanapoishi.

Kauli hiyo imetolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, alipokuwa akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa wajumbe wa Kamati ya Halmashauri Kuu ya CCM, Mkoa wa Tabora.

Alisema kati ya fedha hizo Sh. bilioni tatu zimetumika kujenga hospitali za Wilaya ya Sikonge na Uyui na ujenzi umekamilika kwa asilimia 97.

Mwanri alisema kuwa Sh. bilioni moja zilitumika katika kukarabati vituo vya afya vya Zogolo cha Halmashauri ya Nzega Mji, na Upuge cha Wilaya ya Uyui.

Sh. bilioni 4.8 zimetumika katika ujenzi na ukarabari wa vituo vya afya vya Simbo cha Igunga, Ulyankulu cha Kaliua, Ussoke cha Urambo, Kitunda na Kipili vya Sikonge, Busondo cha Nzega na Ussoke Mlimani cha Urambo.

Vituo vingine ni Igurubi cha Igunga, Maili Tano kilichopo Manispaa ya Tabora, Igalula cha wilayani Uyui na ujenzi wa wodi ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya Wilaya ya Nzega.

Naye Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Urambo, Obed Balola, alizitaka Halmashauri ya Wilaya ya mbalimbali kuongeza juhudi kuandika wananchi wanaojiunga na Mfuko Afya ya Jamii (CHF) ili waweze kupata huduma za afya kwa gharama nafuu.

Alisema Mkoa wa Tabora una ya kaya 421,023 na hadi hivi sasa kuna kaya 5,780 na wananchi 29,713 ndio wananufaika na huduma hiyo.

Balola alisema idadi hiyo ni kidogo jambo ambalo linaonyesha kuwa watu wengi bado hawana uhakika na huduma za afya.

Mbunge wa Jimbo la Manonga Seif Gulamali ameipongeza serikali kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya miradi mbalimbali ikiwamo ya afya.





Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Dk. Aggrey Mlimuka, akizungumza katika ufunguzi wa awamu ya tano na sita ya mafunzo ya kuwajengea na kuwaandaa wanawake kushika nafasi za juu za uongozi, yanayoendeshwa na Chuo Kikuu cha Uongozi Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAMI), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Mbinu kudhibiti ukatili yaanikwa

**Na Godfrey Mushi,** SAME

SERIKALI imesema ili kupunguza ongezeko la matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto hasa ukatili wa kingono katika Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, inakusudia kuimarisha uchumi wa familia na kaya zake.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Same, Benedict Misani, aliyasema hayo jana wilayani hapa, alipokuwa akitoa taarifa kuhusu hali halisi ya ukatili kwa wanawake na watoto Tanzania mbele ya wajumbe wa kamati ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto (Mtakuwwa).

Kamati hiyo inajengewa uwezo na Shirika la Kilimanjaro Women Information Exchange Community Organization (Kwieco) kwa ubia na Taasisi ya Kimataifa ya Friedrich Naumann Foundation for Freedom (FNF).

"Mwongozo wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto, unataka na unaelekeza tupanue mpango wa uimarishaji mifumo ya ulinzi na usalama wa mtoto katika kila halmashauri, tuwe na uhamasishaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama kwa watoto.

"Lipo pia suala la utoaji huduma za msaada wa kisaikolojia kwa familia na watoto waathiriwa wa vitendo vya unyanyasaji na ukatili na hasa tumeelekezwa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za ulinzi na usalama kwa watoto na masuala ya mila na desturi," alisema.

Alisema ukatili wa ngono unaongezeka kulingana na umri wa mwanamke kwa mfano asilimia 11 ya wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 19, walifanyiwa ukatili huo kulinganisha na asilimia 18 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 40 hadi 49 kwa mujibu wa Ripoti ya Upimaji wa Demografia na Afya Tanzania (TDHS 2015/16).

"Kwa hili la unyanyasaji wa kingono, watoto 3 kati ya 10 ambao ni wasichana na mtoto mmoja kati ya saba wa kiume wamefanyiwa ukatili kabla hawajafikisha umri wa miaka 18.

Wakati unyanyasaji wa kimwili ni asilimia 72 kwa watoto wa kike na asilimia 71 ya watoto wa kiume wamefanyiwa ukatili kabla hawajafikisha umri wa miaka 18," alisema.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **WAUNGWANA AUCTION MARTna ADILI AUCTION MART** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limitedwatauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magarina Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika.

Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda uliotajwa tangu kutoka kwa gazeti hili, Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada.

Mnada utafanyika sehemu nyumba, gari na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | LUMUMBA | ADILI AUCTION MART | MAEMBE/T,AGUSTINI | MAEMBE/T,AGUSTINI | NYUMBA-PAGALE | ULONGONI B | 06/03/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 2 | LUMUMBA | WANGWANA AUCTION MART | NAKOS LOGISTICS COMPANY LIMITED | NAKOMOLWA/OBEDI,MA NASE | GMP PICKUP T439CLN | TABATA | 29/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 3 | LUMUMBA | ADILI AUCTION MART | MUNISHI/JOSEPH,HAPPY | NGWALLE JUMA NASSORO | KIWANJA | MBONDOLE | 06/03/2020 SAA 06:01 MCHANA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa mara usomapo tangazo hili.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo na 75% baada ya siku 14 toka siku ya mnada kufanyika na ukishindwa kulipa malipo yaliyobaki mnada utarudiwa na fedha ulizo lipa hazitarudishwa
3. Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe, kumbuka vigezo na masharti kuzangatiwa

**MAWASILIANO**
**WAUNGWANA AUCTION MART 0713077474**
**ADILI AUCTION MART 0716651103**

215639502


# Siku 3 zaongezwa uboreshaji wa daftari la wapigakura Dar

**Na Romana Mallya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imeongeza muda wa siku tatu katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura Mkoa wa Dar es Salaam kutokana na wingi wa watu jijini humo.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa tume iliongeza vituo na ilidhani watu wangejitokeza katika siku saba zilizokuwa zimetengwa awali.

"Sababu ya msingi ni kwamba tulidhani wananchi watajitokeza ndani ya siku saba na vituo tuliongeza na haya ni mazoea ya watu na tarehe 14 ilikuwa Valentine's Day, ikaenda Jumamosi na Jumapili, jana (juzi) tukaona watu wanajitokeza wengi.

"Ninaamini hata leo (jana) watakuwa wengi sana na wakisikia tumeongeza wataacha, lakini kwa nini tumeongeza siku? Tunataka Watanzania hasa vijana wenye umri wa miaka 18 na wale waliohama maeneo yao wajiandikishe," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema wameongeza muda baada ya kupokea maombi mengi kutoka kwa wananchi kutoka maeneo mbalimbali na jiji hilo lina watu wengi.

Dk. Charles alisema kwa kuwa nia ya tume ni kuona kila Mtanzania mwenye sifa ya kupiga kura anapata fursa hiyo, wameamua kuongeza muda hadi Jumapili ikiwa ni awamu ya kwanza ya uboreshaji huo.

Aliwatoa hofu Watanzania kuwa hiyo ni awamu ya kwanza na kwamba itakuja awamu ya pili, hivyo hakuna atakayeachwa nyuma.

Alisema tume imejipanga kutoa elimu kwa wananchi ili kuwakumbusha kuwa ni wajibu wao wale wenye sifa kujiandikisha na kupiga kura ili kuwachagua wagombea wanaowataka.

Kiongozi huyo alisema hakuna atakayeachwa nyuma kwa sababu waliongeza vituo na kufikia 37,714 ili kila mwenye sifa apate haki yake.

Alisema vituo vitaendelea kufunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni na kuwataka Watanzania ambao bado hawajaboresha taarifa zao, wajitokeze.

"Niwakumbushe tu kuwa uboreshaji huu unawalenga makundi matano ambayo ni waliotimiza umri wa miaka 18, wanaokamilisha taarifa zao, wanaoboresha taarifa wakiwamo waliohama maeneo yao ya awali, waliopoteza kadi ya mpigakura au picha kufutika katika kitambulisho na kuwaondoa waliofariki dunia," alisema.

TUME HURU

Kuhusu hoja ya tume huru na watu kukosa imani na NEC, Dk. Charles alisema wao wanayo imani nayo na inafanya kazi zake kwa uhuru.

"Watu wengine wanaweza kudhani tume huru ni ile inayopokea fedha kutoka nje ya nchi kuwa ndiyo ina 'god father' kwa kuwa wanapewa fedha na mataifa ya nje ndiyo tume huru. Watanzania tueleweke maana ya uchaguzi ni kuweka viongozi madarakani watakaowaletea maendeleo," alisema.

**HABARI KITAIFA**

# Huduma bima kutolewa matawi ya NMB

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeanza kutoa huduma za bima katika matawi yake yote 224 nchini kote.

Huduma hii imefuatia uzinduzi wa huduma ya bima kupitia benki (Bancassurance) uliofanyika juzi jiji Dar es Salaam.

Huduma za bima zitakazopatikana katika matawi ya Benki ya NMB ni zile za kampuni za Sanlam Life, UAP, Shirika la Bima la Taifa (NIC), Jubilee, Shirika la Bima la Zanzibar (Zanzibar ( ZIC) na Reliance.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Meneja Mwandamizi wa Bima wa Benki ya NMB, Martin Massawe, alisema uwapo wa matawi ya benki yake katika wilaya zote nchini kutasaidia kukuza sekta ndogo ya bima na kuinua mchango wake katika pato la taifa.

"Tulipata leseni ya kutoa huduma za bima baada ya kupitishwa kwa kanuni za Bancassurance mwaka jana. Kutokana na kupatikana kwa matawi ya NMB katika wilaya zote nchini, tunaamini kupatikana kwa huduma za bima katika matawi yetu kutasaidia kukuza sekta ndogo ya bima," alisema.

Naye Kamishna wa Bima wa Mamlaka ya Bima nchini (TIRA), Dk. Mussa Juma, alisema serikali kupitia taasisi yake inachukua juhudi mbali mbali ili kukuza sekta ndogo ya bima nchini ili mchango wake katika pato la taifa ufikie asilimia tatu ifikapo mwaka 2023.

Hivi sasa sekta ndogo ya bima zinazosimamiwa na Mamlaka ya Bima nchini, huchangia asilimia 0.7 ya pato la taifa.

"Malengo yetu ni kuhakikisha kuwa asilimia 60 ya Watanzania watu wazima wawe wanapata huduma za bima ifikapo mwaka 2024. Tunalenga pia kuhakikisha kuwa asilimia 60 ya Watanzania wote wawe wameweza kuelewa umuhimu wa bima ifikapo mwaka 2024," alisema.

Ili kufikia azma hiyo, kampuni za bima, madalali wa bima, mawakala wa bima na benki zinazotoa huduma za bima zitalazimika kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa Watanzania ili wapate kuelewa umuhimu wa kuziwekea bima mali zao.

Alisema wadau wa bima watalazimika kutumia teknolojia mpya ili kuwafikia watu wengi zaidi, wakiwamo wafanyabiashara ndogo na baba/mama lishe.

Naye Ofisa Mkuu wa wateja binafsi, Biashara Ndogo na za Kati wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, alisema benki hiyo imeshatoa elimu ya bima kwa wafanyakazi wake wapatao 200 ambao wamethibitishwa kumudu utoaji wa huduma za bima kwa wateja.

"Tunaamini ujio wa Benki ya NMB katika kutoa huduma za bima ni game changer (ibadili mwenendo wa sekta) na kuipeleka [sekta] katika viwango vya juu," alisema.

Alisema NMB itatumia uwapo wa vilabu vya kibiashara katika maeneo mbali mbali nchini ili kueneza ujumbe wa umuhimu wa bima.

NMB Business Club ni mahali muafaka pa kuelimisha wafanyabiashara juu ya masuala mbalimbali kuhusu biashara zao. Vilabu vya kibiashara vya NMB vimezinduliwa nchini kote kwa lengo la kutatua changamoto zinazo wakabili wafanyabiashara nchini.

"Kupitia vilabu hivi, tutawafikishia ujumbe wa umuhimu wa kukata bima ya mali zao na biashara zao....Tunafanya pia kazi na wakulima ambao watafikishiwa ujumbe wa umuhimu wa kukata bima kama vile za mazao na nyingine zinazoendana na makundi yao," alisema.

Benki pia itakuwa ikikusanya maoni ya aina za bima zinazohitajika katika maeneo mbalimbali kulingana na mahitaji ya wateja na kuyapeleka katika kampuni za bima.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack (katikati), akiangalia namna madini ya almasi yanavyo kaguliwa ubora wake, katika chumba cha madini ndani ya mgodi wa Mwadui, kabla ya kufanyika kwa mnada wa madini hayo, mkoani humo juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Almasi ya Mwadui kuuzwa kwa mnada

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKOA wa Shinyanga kwa kushirikiana na Wizara ya Madini, wanatarajia kufanya mnada wa madini ya almasi katika Mgodi wa Mwadui ulioko wilayani kishapu, kwa kuuza asilimia tano ya madini yaliyozalishwa na mgodi huo.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa Mkoa huo, Zainab Telack, alipozulu kwenye mgodi huo ili kukagua maandalizi ya mnada wa madini hayo unaotarajiwa kufanyika leo.

Alisema Mkoa wa Shinyanga unakwenda kuweka historia kwa kufanya mnada wa madini hayo kwa mara ya kwanza, akibainisha kuwa serikali na mgodi walikubaliana asilimia tano ya madini yanayozalisha katika mgodi huo, yauzwe kwa wazawa ili nao wanufaike na rasilimali za nyumbani na kuinuka kiuchumi.

"Mkoa wa Shinyanga kwa mara ya kwanza unakwenda kuweka historia katika nchi hii, Februari 21 mwaka huu (leo), tunakwenda kufanya mnada mkubwa wa kuuza madini ya almasi asilimia tano ambazo huzalishwa na Mgodi wa Mwadui.

"Na madini haya yatauzwa kwa wafanyabiashara wazawa tu na siyo watu wa kigeni, lengo la serikali ni kunufaisha wafanyabiashara wa madini na wachimbaji wadogo wanufaike na rasilimali za nyumbani na kukua kiuchumi," alitamba.

Baadhi ya wafanyabiashara wa madini hayo, akiwamo Projects Joseph aliyetembelea mgodi huo ili kuona madini hayo na kujipanga kwa ajili ya mnada, waliipongeza serikali kwa kupigania wazawa kunufaika na rasilimali za nchi.

Meneja Biashara na Mthamini wa Madini ya Almasi kutoka Tume ya Madini, George Kaseza, alisema maandalizi ya mnada huo yanaendelea vizuri na wafanyabiashara wengi wamejitokeza kuangalia madini hayo na wako tayari kwa mnada.

# Ado Shaibu kujitosa ukatibu mkuu ACT

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mawasiliano kwa Umma, Ado Shaibu, ametangaza nia kugombea nafasi ya Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo.

Hadi sasa wanachama wawili Dorothy Semu na Joran Bashange, wameshachukua nafasi ya kuwania nafasi hiyo, huku wengine wakigombea nafasi nyingine katika uchaguzi utakaofanyika Machi, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, baada ya kuchukua fomu za kuwania nafasi hiyo, alisema yupo tayari kushika nafasi hiyo ya utendaji katika kipindi chenye mabadiliko ya kisiasa.

Alisema kwa sasa kuna njama za mara kwa mara kwa kuwafungia wanasiasa, kufuta chama, kubambikia kesi zisizo na dhamana na tishio la kuuawa.

"Kwa mazingira haya naamini ACT -Wazalendo inahitaji Katibu Mkuu anayeelewa hali hii vizuri na atakayelinda chama chetu kwa wivu mkubwa," alisema.

"Tunaishi katika zama ambazo CCM inahofia sana uchaguzi na inatamani kwenye uchaguzi Mkuu ujao kurudia walichofanya kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa," alidai bila kutoa ufafanuzi.

Aidha, alisema anaamini anahitajika Katibu Mkuu ambaye atafahamu kuwa huu ni mwaka wa maamuzi na yeye mwenyewe kuongoza programu za kuongoza umma kudhibiti jambo hilo.

Kwa mujibu wa Shaibu, ACT-Wazalendo inahitaji kiongozi ambaye atafahamu wajibu wa kuwahamasisha, kuwaunganisha na kuwaongoza Watanzania, ikiwa ni pamoja na kuelewa historia ya chama.

# Musoma yakamilisha ujenzi wa madarasa

**Na Sabato Kasika**

WILAYA ya Musoma mkoani Mara, imekamilisha ujenzi wa madarasa 24 yaliyokuwa yakihitajika kwa ajili ya wanafunzi walioanza kidato cha kwanza mwaka huu wa 2020.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Vicent Anney, aliliambia gazeti hili jana kwa njia ya simu kuwa serikali kwa kushirikiana na wananchi imekamilisha ujenzi huo hivi karibuni, na sasa bado vitu vichache kumaliza tatizo hilo.

"Wilaya yangu ina halmashauri mbili za Musoma na Manispaa, ambazo kila moja ilikuwa na idadi tofauti ya uhaba wa madarasa na zote imefanikiwa kumaliza tatizo hilo mapema iwezekavyo," alisema Dk. Anney.

Akifafanua zaidi Dk. Anney alisema Halmashauri ya Musoma ilikuwa na uhaba wa madarasa 13 na Manispaa ya Musoma madarasa 11, ambayo jumla ni 24, tulihamasisha wananchi wakajitolea kwa hali na mali kujenga.

"Katika wilaya yangu, jumla ya wanafunzi 72,280 walichaguliwa kuingia kidato cha kwanza, ndiyo maana kulikuwa na kasi ya ujenzi wa madarasa, ambayo sasa yamekamilika kwa ajili yao," alisema.

Dk. Anney alisema katika idadi hiyo ya wanafunzi waliofaulu kwenda sekondari, 3,480 ni wa Wilaya ya Musoma wakati 3,748 ni kutoka Manispaa ya Musoma ambao jumla yao ni 72,280.

Alisema ukamilishaji huo wa ujenzi wa madarasa ni hatua, nzuri ingawa bado kuna haja ya kuongeza mengine zaidi, ili kuondokana na uhaba huo, ambao umekuwa ukijitokeza kila mwaka.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha kila mtoto aliyefaulu anakwenda sekondari na ndivyo ambavyo tumefanya kwa kuhamasisha wananchi na wadau wengine wa elimu kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa madarasa mapya," alisema.

Mbali na hilo, alisema, sekondari mpya mbili za Busambara na Dan Mapigano, zilianza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza Januari mwaka huu na tayari zimepata vyeti vya usajili.

"Vilevile wakazi wa Kata ya Nyakatende, inayoundwa na vijiji vinne vya Kakisheri, Kigera Etuma, Kamuguruki na Nyakatende yenyewe, wanaendelea na ujenzi wa sekondari ya pili," alisema.

Alisema, ujenzi huo utakapokamilika utasaidia kuondoa usumbufu kwa wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata elimu na pia kupunguza msongamano wao darasani.

# Ataja sifa kupigiwa kura uchaguzi 2020

**Na Mwandishi Wetu,** NKASI

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, amesema mwaka huu unapaswa kuwa maalum kwa ajili ya kuwajali na kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili vinavyosababisha mimba za utotoni, lishe duni, ulawiti, kukosa elimu na aina nyingine za manyanyaso dhidi ya mtoto.

Katika kuhakikisha hilo linatimia, kiongozi huyo wa mkoa amesema wananchi mkoani mwake wanapaswa kuhakikisha wanawachuja wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya mkoa huo kupitia sera zao juu ya kutetea maslahi ya watoto na haki zao katika uchaguzi mkuu mwaka huu.

Wangabo aliyasema hayo juzi katika sherehe za uzinduzi wa mkakati wa miaka mitano (2020-2025) wa kukabiliana na mimba za utotoni mkoani humo zilizofanyika katika Mji Mdogo wa Namanyere, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, zikihudhuriwa na wabunge wa mkoa huo, wakurugenzi, wenyeviti wa halmashauri na wadau wa maendeleo kwa mtoto.

Alisema msingi bora wa makuzi ya mtoto ni elimu, akibainisha kuwa Mkoa wa Rukwa wenye vijiji 339 na kata 97, una vijiji 59 ambavyo havina shule za msingi na kata 25 hazina shule ya sekondari.

Alisema hali inasababisha wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda shule, hivyo kuwa rahisi kurubuniwa na hatimaye kupata mimba za utotoni.

"Mwaka jana tulifanya uchaguzi wa serikali za mitaa, sasa jukumu lao la kwanza hawa viongozi na hao wengine ambao wanataka kuwa wabunge mwaka huu na madiwani wahakikishe kwamba hivi vijiji 59 vyote vinakuwa na shule ya msingi, kampeni zenu kujipanga kwenu kote, piga ua jengeni shule za msingi kwenye vijiji vyenu vyote 59. "Na kule ambako kuna shule ya msingi, hakikisheni kuna vyumba vya madarasa vya kutosha pamoja na madawati, hapo ndipo tutakuwa tunawatendea haki wananchi, lakini siyo tunatafuta uongozi wakati huduma za jamii zimedumaa. Hili ni jukumu kubwa kwa yeyote yule anayetangaza nia au kwa anayetaka kubaki kwenye nafasi yake ya ubunge na udiwani.

"Watoto wanakaa kwenye nyumba ambazo sio rasmi kama mabweni au hosteli wanajipangisha huko, halafu wanajilea, mtoto mdogo ametoka darasa la saba ambaye miaka yote amekuwa akilelewa na wazazi wake, lakini ghafla anaanza kujilea mwenyewe, ajilishe ajipikie, aoge, ajilinde mwenyewe tunawapeleka wapi hawa?

"Ni lazima tujenge mabweni, tujenge shule za sekondari kwenye kata zote 25, hili ni jukumu jingine la viongozi hawa wapya wa serikali za mitaa wakishirikiana na wakurugenzi, madiwani na wabunge wanaotangaza nia.

"Hili ni jukumu kubwa na muwahoji huko, akifika huko unamwambia 'hatuna shule ya sekondari katika kata yetu, tutashirikiana namna gani tujenge shule ya sekondari kwenye hii kata?'" Alifafanua.

Mbunge wa Viti Maalum mkoani Rukwa, Aida Khenan (Chadema), aliwataka wanafunzi wanaopata ujauzito wakiwa shuleni, kutokata tamaa kwa kuwa hata yeye ni mwathirika wa tukio hilo, akieleza kuwa alipata ujauzito akiwa kidato cha tatu, lakini leo ni mbunge.

Takwimu za matukio ya mimba za utotoni zinaonyesha katika kipindi cha kuanzia mwaka 2017 hadi Agosti mwaka jana, Mkoa wa Rukwa ulikuwa na matukio 722 ya wanafunzi kupata mimba.

Kati yake, matukio 171 (24%) yalitokea katika shule za msingi na 551 (76%) yalitokea sekondari huku kwa mwaka 2019 pekee kukiripotiwa matukio 692 ya ukatili dhidi ya watoto mkoani humo.



Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Kakisheri na Kigera Etuma, Musoma Vijijini, mkoani Mara, wakisaidiana na mafundi kuweka renta kwenye moja ya madarasa ya sekondari ya pili inayojengwa, Kata ya Nyakatende juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wanaolima kwenye vyanzo vya maji waonywa

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

SERIKALI wilayani Masasi mkoani Mtwara, imewataka wakulima wilayani humo ambao wanaendesha shughuli za kilimo kwenye vyanzo vya maji kuacha mara moja, kwani zimekuwa chanzo cha uharibifu wa mazingira na miundombinu.

Agizo hilo lilitolewa jana wilayani Masasi na Mkuu wa Wilaya hiyo, Selemani Mzee, wakati wa kikao cha majumuisho ya ziara ya Bodi ya Barabara Wilaya ya Masasi.

Mzee alisema kupitia ziara ya wajumbe wa bodi wilaya ya Masasi, walibaini kuwapo kwa uharibifu wa mazingira pamoja na miundombinu ya barabara kutokana na shughuli za kilimo.

Alisema baadhi ya wakulima wilayani Masasi wamekuwa na tabia ya kufanya shughuli za kilimo kwenye vyanzo vya maji na kando kando ya barabara, hivyo hali hiyo imeathiri kwa kiasi kikubwa kuharibu mazingira na barabara.

"Naagiza wakurugenzi wa halmashauri wawaandikie barua watendaji kata na vijiji ili wawajibike kwa hili kwenye maeneo yao kwa kupiga marufuku kufanya kilimo kwenye vyanzo vya maji," alisema Mzee.

Alisema vyanzo vingi vya maji wilayani humo vimevamiwa na wakulima na vyanzo hivyo vimeshaanza kutoweka, hivyo serikali haitavumilia kuona jambo hilo.

Mzee alisema kila mtu kwa nafasi yake, lazima asimame kidete kugomea suala hilo kwani bila ya kufanya hivyo miundombinu pamoja na mazingira kwa ujumla vitaendelea kuharibika kwa sababu ya shughuli za kilimo.

# Kigogo CCM aonya fitina kwa wanaonyemelea ubunge

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco), limesema limejipanga kumaliza kabisa tatizo la kukatika kwa umeme hadi kufikia mwaka 2025.

Hayo yalisemwa na Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji Tanesco Mkoa wa Arusha, Mhandisi Raimond Seya, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kufunga mafunzo ya kujengea uwezo wahandisi wa matengenezo na mameneja wa shirika hilo wa mikoa na kanda ya kaskazini. Alisema awali kulikuwa na la tatizo la kukatika kwa umeme, lakini wamejipanga kulitatua, kwa kufanya maboresho zaidi kwenye sehemu mbalimbali za umeme.

Aidha, alisema shirika hilo litaendelea kuboresha utoaji wa huduma hiyo, kufikia viwango vya kimataifa ili wateja waridhike na huduma wanazotoa.

"Serikali inapoteza mapato viwandani wakati umeme unapokatika mfano kwenye kiwanda cha kutengeneza plastiki umeme ukikatika wakati wanaendelea kuzalishaji bidhaa wanaharibu materials (vifaa) walivyokuwa wakitumia kutengeneza bidhaa hizo," aliongeza Seya.

Hata hivyo, alisema matarajio yao ni kuhakikisha kila mwananchi ananufaika na huduma ya umeme ambao utakuwa wa uhakika kila siku.

Hata hivyo, alisema kuwa sera ya serikali ni kufikia uchumi wa kati na wa viwanda, hivyo ni lazima waboreshe huduma ya umeme kuwa ya uhakika ili kuwavutia wawekezaji wengi.

Meneja Mwandamizi na Usambazaji wa Umeme wa shirika hilo, Mhandisi Mahende Mgaya, alisema mafunzo hayo yalianza kwa kufuatili na kuangalia chanzo kikuu cha kukatika kwa umeme kuanzia mwaka 2015 na baada ya hapo wataandaa mpango mkakati wa kutatua tatizo hilo.

"Lengo letu ni kuweka mpango mkakati utakaoendana na sera ya nchi, ili kufikia uchumi wa kati na viwanda ni lazima kwanza tuwe na umeme wa uhakika na wa kutosha," alisema na kuongeza:

"Pia usio katikatika mara kwa mara na tukishaboresha mipango yetu, tutawavutia wawekezaji wengi kuja kujenga viwanda hapa nchini kwetu."



Mwenyekiti wa Taasisi ya ECLAT, Peter Toima, akizungumza baada ya kuikabidhi serikali madarasa manne, matundu 16 ya choo, ofisi mbili za walimu na miundombinu ya maji katika Shule ya Msingi Mazinde Toima, Kata ya Loiborsoit, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara jana, ambayo wanafunzi wake walikuwa wanasomea chini ya miti. **PICHA: GIFT THADEY**

# Tanesco kutatua kukatika umeme

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco), limesema limejipanga kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme hadi kufikia mwaka 2025.

Hayo yalisemwa na Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji Tanesco Mkoa wa Arusha, Mhandisi Raimond Seya, wakati akizungumza na waandishi wa habari, wakati akifunga mafunzo ya kujengea uwezo wahandisi wa matengenezo na mameneja wa shirika hilo wa mikoa na Kanda ya Kaskazini.

Alisema awali kulikuwa na la tatizo la kukatika kwa umeme, lakini wamejipanga kutatua tatizo hilo, kwa kufanya maboresho zaidi kwenye sehemu mbalimbali za umeme.

Shirika hilo, litaendelea kuboresha utoaji wa huduma hiyo kufikia viwango vya kimataifa ili wateja waridhike na huduma wanayoitoa.

"Lengo la semina hii ni kuwapa mafunzo wahandisi wetu ili wafanye kazi usiku na mchana, kwa ajili ya kutatua tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara kitendo hicho kinaisababishia serikali ukosefu wa mapato," alisema Seya.

"Serikali inapoteza mapato viwandani wakati umeme unapokatika, mfano kwenye kiwanda cha kutengeneza plastiki umeme ukikatika wakati wanaendelea uzalishaji bidhaa wanaharibu malighafi waliokuwa wakitumia kutengeneza bidhaa hizo," aliongeza Seya.

Matarajio yao ni kuhakikisha kila mwananchi ananufaika na huduma ya umeme ambao utakuwa wa uhakika kila siku.

Alisema sera ya serikali ni kufikia uchumi wa kati na wa viwanda hivyo ni lazima waboreshe huduma ya umeme kuwa ya uhakika ili kuwavutia wawekezaji wengi.

Meneja Mwandamizi na usambazaji umeme wa Shirika hilo, Mhandisi Mahende Mgaya, alisema mafunzo hayo, yalianza kwa kufuatilia na kuangalia chanzo kikuu cha kukatika kwa umeme kuanzia mwaka 2015, na baada ya hapo wataandaa mpango mkakati wa kutatua tatizo hilo.

"Lengo letu ni kuweka mpango mkakati utakaoendana na sera ya nchi, ili kufikia uchumi wa kati na viwanda ni lazima kwanza tuwe na umeme wa uhakika na wa kutosha, pia usio katika mara kwa mara na tukishaboresha mipango yetu, tutawavutia wawekezaji wengi kuja kujenga viwanda hapa nchini kwetu," alisema Mgaya.

# Yaeda Chini sasa kuwasaka wezi wa mifugo

**Na Allan Isack,** MBULU

WANANCHI wa Bonde la Yaeda Chini, wanaopakana na Wilaya za Mbulu mkoani Manyara na Wilaya ya Karatu mkoani Arusha, wamepiga kura ya kuwafichua watu wanaoshirikiana na wezi wa mifugo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga na Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, walisimamia zoezi hilo ili kukomesha wizi wa mifugo kwenye eneo la mpakani mwa wilaya hizo.

Theresia alisema lengo la kupigwa kwa kura hizo ni kukomesha wizi kwenye eneo hilo na zoezi hilo, lilifanyika kwa kuandika majina ya watu wanaodaiwa kuiba mifugo au wanaoshirikiana na wezi kwa ajili ya kukomesha hali hiyo.

Mofuga alisema pia waliwabaini mahalifu walioharibu miundombinu ya alama za mipaka ya bonde hilo, na kwamba walichukua jukumu la kupiga kura kwa kuandika majina ya wahusika wote.

"Hii ndiyo njia sahihi ya kutafuta wahalifu tunaamini hamtaweza kuandika majina ya watu kwa kuwaonea, na matumaini yangu tabia hii itafikia mwisho na wizi huu utafikia kikomo maana wahusika wanajulikana na wakiendelea na tabia hii serikali itawashughulikia," alisema.

Mahongo alisema kwa sababu wao wameteuliwa na kula kiapo kwa kuwatumikia wananchi, hawatakubali kuona wezi wachache wanaharibu amani na kuwasababishia wananchi umaskini.

"Majina haya tutaondoka nayo ili kuyashughulikia, nyie wenyewe mtaona kwa vitendo na wezi hawa wataacha wizi kwani muda siyo mrefu watabainika," alisema.

Awali, baadhi ya wananchi wa eneo hilo walituhumiana kuibiana mifugo ndipo serikali ikaandaa utaratibu wa kupiga kura za siri kwa kuandika majina ya wahusika wa matukio hayo ili kuwabaini wahalifu.

Mkazi wa Kijiji cha Matala, Julius John, alisema ana amini wezi wa mifugo wanashirikiana na mtandao mkubwa wa watu wanaoishi eneo hilo, kuiba na kuuza mifugo hiyo.

John alisema haiwezekani mtu kutoka mbali ya eneo hilo kwenda kuiba mifugo kijijini hapo, kama hana mtandao wa watu wanaoshirikiana nao kutenda uhalifu huo.

# Kisukari Siha changamoto

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

SASA ni rasmi kuwa Hospitali ya Wilaya ya Siha, itaanzisha kliniki maalumu ya wagonjwa wa sukari, baada ya ripoti ya uchunguzi wa madaktari bingwa kuonyesha kuwa kuna wagonjwa wapya 203.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Siha, Dk. Andrew Method, alisema ripoti ya uchunguzi kuhusu ugonjwa huo, inaonyesha kuwa ongezeko la wagonjwa wa sukari katika kata 17 za wilaya hiyo ni kubwa kutokana na mabadiliko ya mtindo wa maisha.

"Katika uchunguzi wetu kati ya watu takribani 3,000 walojitokeza kuchunguzwa magonjwa mbalimbali wakati wa kambi maalum tuliyoifanya wiki iliyopita, tumegundua wagonjwa wapya 203 wa sukari na tunafikiri kuna haja sasa ya kuanzishwa kliniki ya sukari hapa Siha kama serikali itaona inafaa," alisema.

Alisema ugonjwa wa kisukari ni miongoni mwa magonjwa sugu yanayoendelea kuathiri afya za mamilioni ya watu wa nchi nyingi duniani ikiwamo Tanzania.

Kwa mujibu wa Dk. Method, ugonjwa huo hutokea pale ambapo tezi ya kongosho inaposhindwa kutengeneza kichocheo aina ya 'Insulin' au pale mwili unaposhindwa kutumia vizuri kichocheo hicho na kusababisha kuongezeka au kushuka kwa kiwango cha sukari kwenye damu au hyperglycemia.

Alisema ili kuepuka maradhi hayo, wakazi wa Siha wanapaswa kubadili mfumo wa ulaji na kusikiliza na kutii ushauri wa wataalamu kuhusu lishe.

Badala ya kuendelea kula vyakula ambavyo baadaye vinawaletea matatizo ya kiafya na matibabu yake ni gharama kubwa.

Magonjwa mengine yaliyofanyiwa uchunguzi na jopo hilo la madaktari ni pamoja na magonjwa ya macho, ambapo wamegundulika wenye tatizo hilo kuwa 1,812, wagonjwa wa shinikizo la damu 343 na wanaolazimika kufanyiwa upasuaji sasa kuwa ni 64, waliopewa tiba ya miwani 1,362 na watoto wenye uono hafifu 29.

Alisema kwa sasa hospitali hiyo inaendelea kutoa elimu kwa wananchi namna ya kujilinda ili kuepuka kupata magonjwa hayo, kwa kuwa magonjwa hayo yanaweza kuzuilika endapo wananchi watapata elimu.

Kutokana na hali hiyo, amewashauri wakazi wa wilaya hiyo kuzingatia mazoezi ili kuwa na miili yenye ubora na kushindwa kupata magonjwa ya mara kwa mara.

Awali, mmoja wa wafadhili wa kambi hiyo ya matibabu ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Kilimo cha Parachichi ya Africado, James Person, alisema zaidi ya Sh. milioni 20 zimetumika kugharamia matibabu hayo.



Mkuu wa Polisi Dawati la Jinsia na Watoto mkoani Kilimanjaro, Zuhura Suleiman (kushoto), akitoa elimu kuhusu ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi kutoka shule mbalimbali mkoani humo jana. **PICHA: JAMES LANKA**

# Malalamiko ya wamiliki mabasi yamwibua RC

**Godfrey Mushi,** MOSHI

MALALAMIKO ya wamiliki wa mabasi mkoani Kilimanjaro kuhusiana na matatizo ya kiufundi katika mizani ya Njia panda ya Himo, yamemwibua Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, ambaye ametaka kuitishwa kwa kikao maalum cha wadau wa usafirishaji na mamlaka za serikali.

Jana, Mghwira alilazimika kuitisha kikao kidogo cha dharura kwa ajili ya kusikiliza maoni ya baadhi ya wasafirishaji na kupata taarifa fupi ya Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) mkoani hapa.

Akizungumza baada ya kikao hicho, Mghwira alisema amelazimika kuitisha kikao hicho ili kujadili malalamiko ya wasafirishaji kuhusu matatizo yanayolalamikiwa na wamiliki wa mabasi katika mizani ya njia panda.

Katika kikao hicho, alimhoji Meneja wa Tanroads, Mhandisi Ntije Nkolante, kuhusu taarifa ya upimaji wa mabasi na utoaji wa taarifa ambazo hazijajitosheleza juu ya mabasi ya abiria yanapopita kupimwa kwenye mizani hiyo.

"Sasa kutokana na malalamiko niliyoyapata kutoka kwa wamiliki wa mabasi ya abiria na nikamhoji Meneja wa Tanroads mkoa, nimeamua na nimeelekeza kuitishwa haraka kwa kikao kingine kitakachojumuisha wadau wa usalama barabarani, wamiliki wa mabasi na ofisi yangu ili kutafuta ufumbuzi wa jambo hili," alisema Mghwira.

Alisema kabla ya kikao hicho kufanyika, kamati ya ulinzi na usalama pamoja na wadau wote na Tanroads watakwenda kukagua mizani hiyo na kuona utendaji wake wa kazi na kutafuta suluhisho la malalamiko ya wasafirishaji kuhusu mizani hiyo.

Mwaka 2017, Tanroads mkoani Kilimanjaro ilisema walikuwa na kusudio la kufunga kamera za usalama (CCTV) katika mizani zote ili kufuatilia shughuli mbalimbali za utendaji kazi.

Wakala huyo alieleza nia yake nyingine ni kudhibiti mienendo ya vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi watumishi wasio waaminifu.

Ilisema kufungwa kwa kamera hizo kutawaondolea usumbufu wa kufuatilia utendaji kazi katika mizani na kutumia muda mwingi na gharama kubwa, pamoja na kurekodi shughuli zote zinazofanyika.

# Mbunge wa Moshi aibuka kivingine

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

BAADA ya kimya cha muda mrefu cha Mbunge wa Moshi Mjini, Japhary Michael (Chadema), kutoonekana katika majukwaa ya kisiasa, hatimaye kiongozi huyo ameanza kutekeleza ahadi zake, kwa kutoa kompyuta tano alizoahidi katika Shule ya Sekondari ya Karanga.

Mbunge huyo alikabidhi kompyuta hizo jana, zikiwa pamoja na mashine ya kudurufu (printer) kwa uongozi wa shule hiyo.

Katika makabidhiano hayo, Mbunge huyo hakutokea, badala yake aliwakilishwa na Katibu wake, Deogatius Gifford aliyetekeleza jukumu hilo mbele ya Diwani wa Kata ya Shirimatunda Francis Shio.

"Nimekuja kwenu kukabidhi kompyuta tano na printer mashine kama ambavyo aliahidi Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini. Anawashukuru na amenituma niseme yuko pamoja nanyi ila anawaomba muendelee kutoa elimu kwa ajili ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) kwa wanafunzi wetu kama ilivyokusudiwa," alisema.

Alisema kukua kwa Tehama kumeleta mabadiliko makubwa katika nyanja mbalimbali za elimu, maisha, kijamii, kiutamaduni na kiuchumi, hivyo uhitaji wa vifaa hivyo shuleni hapo bado ni mkubwa.

"Tehama imekuwa ni chachu ya maendeleo duniani kote kwa sasa na tunapoelekea katika uchumi wa kati wa viwanda ni vyema tukawaanda wanafunzi wetu katika matumizi ya kompyuta," alisisitiza Mbunge huyo

Mbunge huyo alisema ameanza mchakato wa kutekeleza ahadi zake hasa zinazohusu sekta ya elimu, baada ya kutathmini na kuona kwamba ulimwengu wa sasa wa utandawazi unazilazimisha nchi zinazoendelea duniani kujikita kwa undani katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.




Baada miaka 18, hatimaye TRA yatua rasmi Kilolo



# BUFE

IJUMAA FEBRUARI 21, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



# Kumesheheni raha kitalii, yanayostaajabisha duniani

**Na Mwandishi Wetu,** aliyekuwa DUBAI

DUBAI ni sehemu ambayo nafsi za dunia nzima zinakutanishwa. Sababui hiyo ikitokana na namna nchi hiyo ilivyosheheni mkusanyiko wa watu wa mataifa mbalimbali idadi kubwa ikiwa ni wafanyabiashara.

Ni nchi ndogo iliyoko katikati mwa Mashariki ya Kati, yenye idadi ya watu wasiozidi milioni 3.5, iliyosheheni vivutio kemkemu vya utalii, yenye ustaarabu wa hali ya juu kutokana uhalifu kwao ni 'bidhaa adimu.'

INAENDELEA UK.14

BIASHARA

DUBAI

# Kumesheheni raha kitalii, yanayostaajabisha duniani

• Ghorofa refu ulimwenguni • Maajabu; binadamu, miujiza • Ikulu ruksa; ona bahari bandia • Hakuna trafiki, wala foleni njiani

INATOKA UK.13

Safari yangu ilianza saa 10: 30 kuelekea Dubai International Airport ambako ni umbali wa maili 2,750 kutoka Uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Ni mwendo wa saa tano kuwasili Dubai, kwa ndege hiyo kubwa yenye uwezo wa kubeba zaidi ya abiria 450. Saa nne usiku tayari ilishafika.

**MSHANGAO UNAANZA**

Moja ya vilivyonishangaza ni uwanja ni mkubwa sana na idadi ya wageni wanaowasili uwanjani nayo kubwa sana. Uwanja umejaa ndege nyingi zinazoruka na kutua kwa wakati mmoja na inawachukua abiria wastani wa dakika 10 kutoka kwenye ndege hadi eneo la kutoka uwanjani.

Hapo nyenzo inayowasaidia ni kuwepo magari maalum ya kusafirisha abiria kutoka kwenye ndege, kuwapeleka sehemu ya kutokea.

Kivutio kingine, uwanjani ni licha ya kupambwa na ndege za mashirika mengine makubwa kama Fly Dubai, ndege kubwa za Shirika la Ndege la Emirates, ambalo ndilo nilisafiri nalo na linakadiriwa kuiwa ndege kufika 275, ndio kivutio kikuu; zimo ndege aina ya Boeing 165 na Airbus 110.

**NILIPOINGIA JIJINI**

Lingine la kuvutia Dubai, ni namna jiji lilivyopambwa kwa barabara za juu karibu kila eneo, kiasi kwamba siyo rahisi kukuta foleni hata dakika moja katika maeneo yote yake.

Barabara zimejengwa kwa ustadi mkubwa, makutano yote yamejengwa katika barabara za juu, zinayawezesha magari sita ya upande mmoja kwenda na mengine sita yanayorudi kupita kwa kasi, hata kumaliza foleni na kuifanya Dubai kuwa ya kipekee.

Ni eneo linalotengeneza mvuto kwa kutazama namna magari ya kila upande yanavyopishana kwa kasi, bila ya kusababisha msongamano.

Miundombinu yake na hasa barabara na daraja, Dubai imejitahidi kuweka barabara za juu kila sehemu waliyoona inaweza kuzaa msongamano, kiasi kwamba unaweza kutoka uwanja wa ndege hadi hotelini kwako bila kusimama hata sekunde.

Jambo lingine la kushangaza Dubai, ni kwamba huwezi kuona gari kuukuu, mengi ni mapya na ya kifahari na nilipotaka kufahamu sababu, mwenyeji wangu aliniambia uchumi umestawi na serikali haiwatozi kodi kubwa wananchi wanapoyaagiza.

"Hapa huwezi kuona gari kuukuu na hutaliona mpaka unaondoka, kwa sababu gari likikaa mwaka au miaka miwili mtu anaweza kuagiza lingine kwa sababu ya unafuu wa kodi," anasema.

**HAKUNA TRAFIKI**

Kivutio kingine cha kufurahisha, ni kwamba si rahisi kukuta askari wa usalama barabarani anayeongoza magari au askari wa kawaida akiranda mtaani, ilivyo kawaida kwenye miji mingine mikubwa duniani.

Mwongoza watalii niliyeambatana naye, aliniambia kuwa zimewekwa kamera kila umbali wa kilomita moja barabarani, hivyo madereva wanajiongoza kwa kuwa adhabu ya kuzidisha mwendo ni kubwa.

Anasema, licha ya kutoonekana askari katika mji huo kiwango cha uhalifu kiko chini sana na iwapo mtu atafanya uhalifu askari huwasili haraka kwenye eneo la tukio kufanya kazi yao kudhibiti chochote cha kiusalama.

"Ukizidisha mwendo ulioweka wa adhabu ni Dola za Marekani 150 (Sh. 330,000) sasa watu wanajisimamia wenyewe hakuna anayependa kutoa kiasi hicho cha pesa hapa sheria inafanyakazi sawasawa watu wanaogopa kufanya makosa," anasema.

Katika raha hiyo ya siku saba za utalii Dubai, sikumwona askari awe wa usalama barabarani au wa kawaida, mwanajeshi, hata mgambo. Ustaarabu umetamalaki.

Nilipomdadisi mwenyeji wangu kulikoni hali hiyo hakuna askari, aliniambia wapo, lakini wanafanya kazi zaidi za kuendeshea ofisini, kwani barabarani kila mtu anajisimamia na maeneo yote ya mji yana kamera, hivyo si rahisi kufanyika uhalifu.

Ingawa siku zote hizo nilikuwa nazungushwa kila kona ya nchi, bado nilikuwa makini kutaka kujiridhisha kama kweli hakuna askari barabarani na sikufanikiwa mpaka nilipopanda ndege, kurejea jijini Dar es Salaam.



Watalii wakiwa kwenye bahari ya kutengenezwa na 'Marine Parks' iliyoko katikati ya mji wa Dubai. **NA MPIGA PICHA WETU**

> **Mandhari ya kuvutia sana nimependa sana huu ubunifu mkubwa, kuleta bahari katikati ya mji ni wazo la ajabu kabisa huwezi kuamini hata kidogo.**

**ILIVYO DUBAI**

Dubai sehemu ya muunganiko wa mataifa saba yanayounda United Arab Emirates (UAE), ambazo ni Dubai, Abudhabi, Shalja, Agman, UmAlqudium, Fujiarah na Ras Al Khaima, ambayo yanazungumza Kiarabu.

Mji mkuu wa mataifa haya ni Abudhabi, ambao unaelezwa kuwa na akiba kubwa ya mafuta ndani ya UAE. Ni mwendo wa nusu saa kutoka Dubai kuufikia mji huo.

Kuna cha mshangao ulioko, ni namna ruksa iliyoko kwa kiongozi wa taifa, Sheikh Mohamed Bin Rashid, alivyotoa uhuru kwa watalii na raia wa kawaida kufika kwenye makazi yake maarufu kama 'Zabir Palace' kwa ajili ya kupiga picha na hata kupiga soga.

Mamia ya watalii wamekuwa wakifika kwenye makazi hayo kupiga picha, bila ya kuvuka kizuizi kinachoelekea kwenye geti kubwa yaliko makazi rasmi kupiga soga na picha kadri wanavyotaka, pasipo kubughudhiwa na mtu.

Mwongoza watalii Mohamed, anayeniambia amefanya kazi hiyo kwa zaidi ya miaka 20, anasema kilichosababisha Sheikh Mohamed kutoa uhuru wa kwenda kwenye makazi yake, ni baada ya kusikia maombi mengi ya wanaotaka kumjua, hasa alivyoleta mageuzi makubwa nchini humo kwa muda mfupi.

"Sheikh Mohamed ni mtu wa watu, ni mtu anayefanya mambo makubwa kwa nchi yake, lakini yuko kawaida sana, aliposikia watu wengi wakiwamo watalii wakitaka kujua yalipo makazi yake, alisema 'waacheni watu waje' ndipo ukaanza utaratibu huo," anaeleza Mohamed.

**HAKUNA UCHAGUZI**

Licha ya kuwapo maenedeleo makubwa, nchi hiyo haina mfumo wa kuwa na uchaguzi na mmoja wa wenyeji wa Nipashe, katika ziara yake huko, anasema wananchi wameridhika na kutohusishwa na hatua hiyo ya demokrasia, badala yake wamejikita kwenye uzalishaji mali, biashara na uchumi kwa ujumla.

"Kila taifa ndani ya UAE lina kiongozi wake na kiongozi wa jumla wa UAE kwa sasa ni Sheikh Khalifa. Iwapo litatokea lolote wakataka kupata kiongozi mwingine, wanakaa hawa masheikh wa mataifa yaliyounda UAE wanachagua kiongozi wao wenyewe," anasema.

**BAHARI BANDIA**

Maajabu mengine ya Dubai, ni namna walivyotengeneza bahari bandia katikati ya mji, kwa kuchimba kiasi cha kilomita nne na kuunganishwa eneo na maji ya bahari, kisha kukatengenezwa eneo maarufu kwa watalii kwa jina la Marine Parks.

Hapo pana la kushangaza na



Watalii kutoka mataifa mbalimbali duniani, wakiwa kwenye jangwa mashuhuri kwa utalii, Dubai.

inamchukua mtu muda kuamini 'bahari bandia' katikati ya jiji kutokana na ukubwa na mwonekano. Hapo pamesheheni watalii wanaoshangaa.

Mtalii mmoja kutoka Serbia, Abela Sakitasna tuliyekuwa naye kwenye boti tukitalii kwenye bahari hiyo bandia, alinieleza kwamba hata yeye hakuamini kirahisi alipoambiwa kuwa hiyo ni kazi ya binadamu na kwamba si eneo la asili.

"Mandhari ya kuvutia sana nimependa sana huu ubunifu mkubwa, kuleta bahari katikati ya mji ni wazo la ajabu kabisa huwezi kuamini hata kidogo," alieleza mtalii huyo,

Vivutio vya utalii Dubai na watalii wanaofurika hasa msimu wa baridi kutoka mataifa mbalimbali duniani ni wengi sana.

Mbali na eneo hilo, mji huo una fukwe za nyingi, bustani za kushangaza, majengo marefu zaidi duniani na mchanganyiko wa watu wa jamii zote duniani.

Kuna kivutio cha kipekee, hapo ni bustani ya maajabu maarufu kama Miracle Garden, kama inavyojieleza kwa jina lake. Ni bustani ya maajabu kutokana na ustadi na ubunifu mkubwa uliotumiwa na wataalamu kuitengeneza.

Ni kivutio kikubwa cha watalii hasa msimu wa baridi kwenda kushuhudia usanifu wa kipekee na kustaajabisha, uliofanywa na wajenzi mahiri duniani.

Mmoja wa watalii kutoka nchini Lithuania, Jane Brendes, aliniambia kuwa maishani mwake hajawahi kuona bustani inayostaajabisha kama hiyo, iliyosheheni kila aina ya maua yenye mambo tofauti na ya kuvutia.

"Hii ni ajabu kweli. Huu ni ujuzi uliofanywa na watu wanaoipenda kazi yao, kuchanganya maua mazuri kwa kiwango hiki na kuwa na maumbo ya kushangaza. Ni jambo lenye kuleta mvuto nilikuwa nasikia 'Miracle Garden' nashukuru nimeona mwenyewe," anasimulia mtalii huyo.

Eneo lingine lenye mvuto wa ajabu ni jangwa lililoko umbali wa kilomita 40 kutoka jijini, ambako watalii hutembelea huko msimu wa utalii kuona wanyama mbalimbali kama ngamia, kwenye eneo maarufu kama 'Dubai Sunset Desert Safari.'

Hapo pamekuwa mvuto wa kipekee, hasa namna magari yanavyosafiri ndani ya jangwa, kutokana na kuwa na miinuko mikubwa na miteremko mikali, kiasi kwamba mtalii anaweza kudhani gari linaanguka.

Kutokana na hali hiyo, sasa yanapelekwa magari ya kisasa yanayosukuma magurudumu manne yaani 'four wheel drive' kwani wenyeji wanasema magari mengine hayawezi kufika maeneo husika yanayolengwa.

### MAENEO YA AJABU

Maajabu mengine ya Dubai ni kitu kinachoitwa La Perle. Ni ukumbi wa maonyesho wenye maajabu ya kushangaza duniani, ukiwa na jumla ya viti 1,300 uliojengwa chini ya hoteli. Umetengenezwa kwa nakshi za ajabu, kiasi cha kushangaza wengi wanaofika kushuhudia maonyesho ya sanaa yanayofanywa kwenye ukumbi huu.

Hapo kuna bwawa la kuogelea lililoko kwenye ukumbi huo ni la maajabu, kwani wasanii wamekuwa wakizama na wasionekane walikotokea.

Katika onyesho la hivi karibuni, jumla ya watu zaidi ya 1,000 waliokuwa kwenye ukumbi huo, walishikwa na butwaa kuona mmoja wa vijana waliokuja kama watazamaji, kutoswa kwenye bwawa hilo na kutoonekana tena.

Umati waliokuwa kwenye ukumbini wakiwa wanasubiri kuona nini kitatokea, walishangaa baada ya dakika 20 kijana huyo kutokea kwenye paa la ukumbi huo, hali iliyozidisha mvuto kwenye onyesho hilo, hivyo kusababisha shangwe.

Maporomoko ya maji kwenye ukumbi huo, ni maajabu ya kusisimua, kwani kuna wakati hutokea maporomoko ya maji kutoka kwenye kona mbalimbali za jingo, hilo kiasi cha kusababisha maji kujaa kuanzia kwenye bwawa la kuogelea lililojengwa kwenye eneo hilo, kisha yanatoweka katika mazingira ya kutatanisha na ajabu.

Mtalii kutoka Hispania, Berbas Bornos, aliyehudhuria onyesho hilo, aliniambia kuwa wahandisi waliojenga ukumbi huo wamekwenda mbele zaidi kwa namna ulivyonakshiwa kwa teknolojia na ubunifu wa ajabu.

"Nimeshuhudia mambo mengi ya ajabu, lakini ukumbi huu ni aina yake na kwangu mimi yanayofanyika hapa ni maajabu, kweli ni maajabu na katika akili ya kawaida inashangaza sana," anasema.

Dubai Parks and Resorts ni eneo lingine la burudani la maajabu ya kuvutia maelfu ya watalii kutoka mataifa mbalimbali duniani, yaliyomo ndani ya eneo hilo maarufu lililoko kilomita 25 kutoka katikati ya jiji.

Ndani ya eneo hilo kuna majengo yaliyosheheni maajabu mbalimbali likiwamo lile maarufu kama Dream works. Kwa uhakika hili ni eneo lililojaa maajabu mbalimbali kiasi kwamba mtalii hujiona kama yuko sayari nyingine.

Ndani ya jengo la 'Dream Works' kama linavyojitambulisha kweli kazi za ajabu zimefanyika kwa ustadi mkubwa, maajabu ambayo mtu hawezi kuamini kwamba binadamu anaunda vitu vya kustaajabisha kwa kiwango hicho.

Watalii wanaoingia ndani ya jengo hilo, hutembezwa chini ya ardhi kulikowekwa sanamu mbalimbali wanayozungumza na kufanya shughuli, mithili ya binadamu na wakati mwingine inatisha kuangalia, kwani maeneo mengi ni giza.

> **"Nimeshuhudia mambo mengi ya ajabu, lakini ukumbi huu ni aina yake na kwangu mimi yanayofanyika hapa ni maajabu, kweli ni maajabu na katika akili ya kawaida inashangaza sana.**

Mfano chini ya ardhi kwenye eneo hilo mtalii anayezungushwa kwa magari maalum yanavyosukumwa na umeme, anakutana na bendi za muziki za sanamu ambazo mtu anaweza kudhani watu halisi, kumbe sanaa.

Kwingine kunakoifanya Dubai kuwa na majabu ya kitalii kutoka kinakoitwa Global Village, eneo lenye ukubwa wa wilaya nzima. Hapo ndani yake kuna maduka ya kila taifa duniani yanayouza bidhaa zinazotengenezwa na mataifa hayo.

Ni eneo linalopata watalii wengi zaidi, kutokana na mvuto wake hasa bidhaa zinazopatikana kwa wingi na kama panavyojitambulisha kwa jina la 'Global Village' kweli ni kijiji cha dunia kutokana na maelfu kwa wafanyabiashara wa mataifa mbalimbali walivyokusanyika kuweka maduka yao katika msimu wa baridi unaoanzia Novemba hadi Aprili ya kila mwaka.

### JENGO REFU

Kwa watalii wengi wanaotembelea Dubai hawawezi kuondoka bila kufika jengo refu kuliko yote duniani maarufu kama 'Burji Khalifa' lenye ghorofa zipatazo 160 ndani kumesheheni mambo mengi ya kuvutia.

Ni eneo ambalo muda mwingi lina msongamano wa watu wanaofurika kutaka kupata fursa ya kufika kileleni mwake.

Pia kuna eneo lingine jirani la Dubai Shopping Malls ambalo lina ghorofa tatu na maduka yanayoelezwa kufikia 1,250 yaliyosheheni bidhaa mbalimbali kila mahali duniani.

Kwa watalii kutoka mataifa mbalimbali duniani, ni eneo ambalo wanakutana na msongamano wa ama wakiingia na kutoka, kwani ni eneo mtu anaweza kupata kila anachokitaka. Ama kweli Dubai, kuna maajabu ya utalii duniani.

UCHUMI

# Baada miaka 18, hatimaye TRA yatua rasmi Kilolo

- DC: Kazi kwenu, changamkia fursa
- Mwisho safari kufuata huduma km.40



Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah na viongozi wengine wakiwa ndani ya ofisi ya TRA baada ya uzinduzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Sabato Kasika**

WILAYA ya Kilolo iliyopo mkoani Iringa, imepata ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ili wananchi waweze kulipa kodi za serikali kwa karibu nao, badala ya ilivyokuwa awali kufuata huduma hizo mbali.

Uzinduzi wa ofisi hizo za TRA, ulifanywa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Asia Abdalah, Februari 7 mwaka huu na kusema, kuwapo ofisi za TRA ni hatua nzuri, itakayoongeza ukusanyaji wa mapato ya wilaya na mkoa kwa ujumla.

Asia anaamini kusogeza huduma za ulipaji kodi karibu na wananchi, kutachochea ari ya ulipaji kodi kwa wananchi na hatimaye kukuza uchumi wa nchi.

"Hapa kwetu kuna rasilimali nyingi zinazoweza kukuza uchumi kuanzia kwenye kilimo cha mazao ya misitu, chai, matunda, ufugaji, utalii na shughuli nyingine nyingi za kiuchumi," anasema Asia.

Mkuu wa Wilaya anasema, kilichobaki sasa ni wananchi kujisajili, ili kupata namba ya mlipa kodi (TIN), walipe kodi inayotakiwa kwa wakati, pia kutunza kumbukumbu za kibiashara na kutoa risiti kwa mauzo wanayofanya.

"Nitoe rai kwa wafanyabiashara wote wa wilaya yangu kwamba, mtumie fursa hii ya uwepo wa ofisi za TRA kupata elimu ya kodi na kulipa kodi kwa wakati, ili kukuza uchumi wa wilaya na kushirikiana na watumishi wa TRA kupata elimu ya kodi na kulipa kodi kwa wakati," anasema.

> **"Hapa kwetu kuna rasilimali nyingi zinazoweza kukuza uchumi kuanzia kwenye kilimo cha mazao ya misitu, chai, matunda, ufugaji, utalii na shughuli nyingine nyingi za kiuchumi.**



Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah, akizungumza katika uzinduzi wa ofisi za TRA wilayani mwake.

Anasema, kabla ya kuwapo ofisi hiyo, wafanyabiashara wa Kilolo walikuwa wakisafiri umbali mrefu wa kilomita 40 kwenda kulipa kodi Iringa Mjini na kwambam changamoto hiyo sasa imeisha.

"Sasa wameondokana na usumbufu huo wa zaidi ya miaka 18, ambao walikuwa wakiupata. Niwapongeze kwa kutambua umuhimu wa kulipa kodi ya serikali kwa kusafiri umbali wote huo kwa ajili ya kulipa kodi," anasema.

"Sasa wameondokana na usumbufu huo wa zaidi ya miaka 18 ambao walikuwa wakiupata. Niwapongeze kwa kutambua umuhimu wa kulipa kodi ya serikali kwa kusafiri umbali wote huo kwa ajili hiyo," anasema.

### KILOLO ILIVYO

Mkuu huyo wa Wilaya, Asia, anasema kwa upande wa Kaskazini Mashariki, Kilolo inapakana na Morogoro na Kusini inapakana na Wilaya ya Mufindi, wakati Magharibi inapakana na Iringa Vijijini.

Anasema, Kilolo ina tarafa nne anazozitaja kwa majina ya Mazombe, Mtandika, Kilolo na Ukwega, huku baadhi ya kata zikiwa ni Bagamoyo, Dabaga, Idete, Ilula, Nyalumbu, Image, Irole, Mahenge, Mtitu, Udekwa, Uhambingeto, Ukumbi, Ukwega, Ibumu na zaidi ya vijiji 100.

"Wilaya ilizinduliwa rasmi mwishoni mwa mwaka 2009 na Rais wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete na kuipongeza halmashauri ya wilaya kwa ujenzi wa ghorofa la halmashauri," anasema.

Kiuchumi, asilimia 90 ya wakazi wa Kilolo wanajishughulisha na kilimo cha mazao mbalimbali ya chakula na biashara kama vile; viazi, njegere, mahindi, maharage na wengine wanapanda miti ya mbao kwa ajili ya biashara.

"Pamoja na shughuli hizo za kilimo cha mazao ya chakula na biashara, hatukuwa na ofisi ya TRA kwa miaka yote zaidi ya 18 tangu wilaya yetu ilipoanzishwa, lakini hatimaye sasa tumeipata," anasema.

### NENO LA TRA

Katika salamu zake wakati wa uzinduzi wa ofisi hizo, Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa TRA, Alice Lukindo, anasema wana jukumu la kusimamia na kutekeleza sheria za kodi kwa kukadiria, kukusanya na kuhesabu mapato ya serikali.

Akizungumza kwa niaba ya Kamishna Mkuu wa TRA, Lukindo anasema, hatua ya kufungua ofisi Kilolo ni kutaka kuongeza wigo wa walipa kodi na huduma za ulipaji kodi kwa Watanzania zaidi.

Meneja wa TRA Mkoa Iringa, Lamson Tulyanje, anasema, mamlaka hiyo imefungua ofisi zake katika wilaya ya Kilolo kwa ajili ya kusogeza huduma zake karibu na wananchi walipa kodi.

"TRA itatumia ofisi za Kilolo kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato ili kufikia lengo la mkoa kwa mwaka wa fedha 2019/2020, mkoa wa Iringa uliwekewa kukusanya Sh. bilioni 71.3 kama mapato ya ndani," anasema Tulyanje.

Anasema, ni uamuzi unaotarajiwa kuongeza ukusanyaji mapato mkoani Iringa, kwa vile wafanyabiashara hawatasafiri tena umbali mrefu, ambao kwa namna moja au nyingine, huenda ulisababisha usumbufu kwao.

### WIGO KODI

TRA kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango inahimizwa kupanua wigo wa kodi kwa kuongeza idadi ya walipa kodi na kuibua vyanzo vipya vya mapato na kujenga mazingira rafiki kwa watu wengi zaidi kulipa kodi.

Hivyo ndivyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli anavyotaka, lengo la kufanya hivyo likiwa ni kuongeza makusanyo ya kodi badala ya kukamua walipa kodi wachache.

Kwamba kupanua uwigo wa kodi na kuweka viwango vya kodi vinavyolipika na vitakavyowavutia watu wengi zaidi kulipa kodi na hivyo kusukuma mbele maendeleo ya Tanzania na wananchi wake kwa ujumla.

Anaitaka TRA kurekebisha dosari zote zilizopo, katika ofisi zao ikiwa ni pamoja na kuwaondoa watumishi wanaoonekana kuwa kikwazo cha kutekeleza mipango ya serikali.





Wananchi wa Kata ya Nsalaga, jijini Mbeya wakiwa katika kusanyiko la kufanya harambee ya kuchangisha pesa kwa ajili ya kufanya ukarabati wa Shule ya Msingi Nsalaga jana. **PICHA: KENNETH NGELESI**

# CCM yakerwa wizi dawa za serikali

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, imekerwa na taarifa za wizi wa dawa za serikali unaofanywa na baadhi ya watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Rungwe ya Makandana ambao unadaiwa kupunguza ufanisi wa utoaji wa huduma za afya.

Kamati hiyo ilionyeshwa kukerwa na taarifa hizo juzi wakati ilipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la kutolea huduma za mama na mtoto ambapo taarifa hizo zilitolewa na Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila.

Akitoa taarifa hizo, Chalamila alisema serikali imewekeza fedha nyingi kwenye uboreshaji wa huduma za afya kwenye hospitali hiyo, lakini baadhi ya watumishi hasa wafamasia wanaiba dawa na kuzipeleka kusikojulikana.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, imeundwa kamati ya kuratibu uingiaji na utokaji wa dawa katika hospitali hiyo, huku akitahadharisha kuwa muda sio mrefu ataanza kuwachukulia hatua za kisheria wahusika wa wizi huo. "Hii hospitali inakabiliwa na kashfa ya wizi wa dawa, sasa mimi naendelea na uchunguzi wangu na sitaona shida kuwasweka ndani wafamasia wote wa hospitali hii, haiwezekani wananchi wanapata shida lakini wao wanachezea dawa," alisema Chalamila.

Aliwataka viongozi wa Wilaya ya Rungwe kuhakikisha wanawasimamia vizuri watumishi wa hospitali hiyo na vituo vingine vya serikali vya kutolea huduma za afya ili kuepuka kashfa hiyo kuendelea. Baada ya maelezo hayo ya Chalamila, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, alisema taarifa hizo za wizi wa dawa ni mbaya na zinaichafua hospitali hiyo ambayo ni ya serikali.

Alisema aliwataka viongozi wa serikali kukaa na watumishi wa hospitali hiyo na kuzungumza nao kuhusu mambo mbalimbali ikiwamo kuwakumbusha maadili ya kazi yao.

Alisema wajumbe wa kamati hiyo walifurahishwa na ujenzi wa miundombinu ya hospitali, lakini taarifa za wizi wa dawa zili-wakatisha tamaa na hivyo kuna kazi ya ziada inatakiwa kufanyika ili tabia hiyo isijirudie.

"Sisi wenyewe watu wa chama tunatakiwa kukaa na hawa watumishi, tuongee nao kuhusu jambo hili, hizi taarifa sio nzuri hata kidogo maana kitendo cha kuiba dawa inamaana wanataka wagonjwa wakose huduma," alisema Mwakasole.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika hospitali hiyo, Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Anosisye Mwasege, alisema serikali ilitoa Sh. milioni 400 kwa ajili ya mradi huo na kwamba mradi huo umebaki kidogo kukamilika.

Alisema maeneo yaliyobakia ili kulikamilisha ni kupachika milango ambayo tayari imeshatengenezwa na kuingiza umeme pamoja na vitanda ili lianze kutumika.

Hivi karibuni, Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, aliibua wizi wa dawa katika hospitali hiyo ambapo alibaini kuwa dawa zinatolewa bila taarifa za maandishi.

## Wakulima na wauza viazi wataka barabara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA na wafanyabiashara wa viazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuwasaidia kuboresha miundombinu ya barabara kwa maelezo kuwa ubovu wa miundombinu hiyo unasababisha kuporomoka kwa thamani ya zao hilo.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wakulima wa Kata ya Santiliya walisema wanalazimika kuuza viazi vyao kwa Sh. 3,000 kwa debe moja kutokana na wanunuzi kusingizia gharama za usafirishaji.

Mmoja wa wananchi hao, John Shilabhi, alisema barabara nyingi katika eneo hilo hazipitiki kutokana na kuwa na mashimo ambayo wenye magari wanahofia kwenda na wanaoenda wanatoza gharama kubwa za usafiri.

"Viazi ni tofauti na mazao mengine, hatuwezi kuvihifadhi mpaka barabara zitakapotengamaa vitaoza, kwa hiyo tunalazimika kuuza hata kama bei ni ndogo, tunawaomba Tarura watusaidie japo kwa kutengeneza maeneo korofi," alisema Shilabhi.

Alisema kuna baadhi ya viazi ambavyo wanapanda sasa hivi lakini kutokana na ubovu wa barabara hizo wanashindwa kusafirisha mbolea kutoka mjini kwenda kwenye mashamba yao.

Mmoja wa wanunuzi wa viazi hivyo, Zacharia Mwazembe ambaye ni mkazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani hapa, alisema hivi karibuni gari alilokuwa amekodi kwenda kubeba viazi lilikwama kwa muda wa wiki moja kutokana na ubovu wa barabara katika Kijiji cha Sanje.

Alisema barabara hiyo ni mbovu na inasababisha wanunuzi wengi kuogopa kwenda kununua viazi hivyo wakihofia usafirishaji kuwa mgumu.

# RC aamuru kukamatwa wafyatua tofali shuleni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata wananchi walioiovamia eneo la serikali na kuanza kufyatua tofali na kukata miti inayomilikiwa na Shule ya Msingi Pambogo katika Kata ya Iyela jijini Mbeya. Aidha, ameliagiza jeshi hilo kuwasaka watu waliotelekeza makontena zaidi ya 20 kwenye eneo hilo ambayo baadhi yamefungwa na hayajulikani yana kitu gani ndani, ambapo alisema ndivyo wanavyoanza kuvamia maeneo ya serikali.

Chalamila alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Shule ya Msingi ya mchepuo wa Kiingereza ijulikanayo kwa jina la Dk. John Magufuli inayojengwa katika eneo hilo ambalo zamani ilikuwa ni eneo la hifadhi ya uwanja wa ndege wa zamani.

Chalamila alisema watu hao wakipatikana wawekwe ndani na wahojiwe ili waeleze aliyewapa kibali cha kulitumia eneo hilo ambalo ni la wazi na serikali ililitenga kwa ajili ya shughuli zake.

"Mtafute aliyefyatua tofali hizi na mmweke ndani, asipoonekana hizi tofali zote lazima zitaifishwe na zitumike kwa ajili ya ujenzi wa shule yetu hapa, tutazitumia hata kujenga baadhi ya miundombinu midogo midogo," alisema Chalamila.

Alisema maeneo mengi yaliyokuwa ya wazi ndani ya jiji hilo yalishavamiwa na baadhi ya watu ambao wamejenga nyumba za kuishi na wengine wamejenga majengo ya vitega uchumi na hivyo serikali haikuwa tayari maeneo yake kuendelea kuvamiwa," alisema Chalamila.

Vilevile, Chalamila aliuagiza uongozi wa jiji hilo kuanza ujenzi wa shule maalumu ya sekondari itakayokuwa inapokea wanafunzi wanaofaulu kutoka kwenye shule za msingi za mchepuo wa Kiingereza.

Alisisitiza kuwa lengo la serikali ni kuliwezesha Jiji hilo kuwa na shule za msingi za mchepuo wa Kiingereza zisizopungua 10, ili halmashauri zingine nchini ziwe zinatuma wataalamu wake kujifunza uendeshaji wa shule hizo.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa Shule hiyo ya Msingi ya Dk. John Magufuli, Fundi Mkuu wa Kikosi cha Itende JKT, Mteule Daraja la Pili, Manfred Ngonyani, alisema wataikamilisha shule hiyo ndani ya miezi mitatu na kukabidhi. Ngonyani alisema wameshakamilisha ujenzi wa msingi wa majengo mawili ambayo yatakuwa ni madarasa na jengo la utawala na wameshamwaga vifusi na sasa hivi wanaendelea kushindilia.

"Tunapata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa uongozi wa Jiji la Mbeya na kama ushirikiano huu utaendelea kuwa hivi basi tutamaliza kazi hii hata kabla ya muda wa makubaliano kwa sababu mpaka sasa tupo mbele ya muda," alisema Ngonyani.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Oscar Kapinga, ambaye ndiye Ofisa Elimu wa Jiji hilo alisema fedha zinazotumika kujenga shule hiyo zinatokana na faida iliyopatikana kwenye shule mbili za aina hiyo ambazo ni Mkapa na Azimio.

Alisema kutokana na uendeshaji wa shule hizo, wamepata uzoefu wa kutosha ambao utawawezesha kuziendesha shule zingine zote zitakazoanzishwa.





# Wanafunzi 1,000 watumia matundu matatu ya vyoo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANAFUNZI zaidi ya 1,000 wa Shule ya Msingi Ipagala jijini Dodoma, wamehamia kutumia vyoo vya walimu vyenye matundu matatu kujisaidia baada ya kutitia kwa vyoo vyao kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

Nipashe ilizuru kwenye shule hiyo na kushuhudia wanafunzi wakigombania kutumia matundu hayo matatu, hasa wakati wa mapumziko ya asubuhi.

Gazeti hili pia lilibaini walimu 43 wa shule hiyo wamelazimika kutovitumia vyoo hivyo ili kuwapisha wanafunzi. Sasa walimu hao wanatumia choo cha mwalimu anayeishi karibu na shule hiyo.

Kutokana na madhara hayo ya mvua, Halmashauri ya Jiji hilo, imelazimika kuchukua Sh. milioni 20 za ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule hiyo kujenga vyoo ili kunusuru afya za wanafunzi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mchumi wa Halmashauri hiyo, Shaban Juma, alisema wamelazimika kufanya hivyo ili kuwanusuru wanafunzi kwa kuwa hata vyoo wanavyotumia kwa sasa ni vichache kulinganishwa na idadi yao.

Alisema wanajenga vyoo vya dharura ili kuondokana na adha hiyo ambayo wanafunzi wamekuwa wakisukumana kuwahi chooni kutokana na uchache wa matundu.

"Naomba wazazi wasiwe na wasiwasi, ndani ya wiki mbili vyoo hivyo vitakuwa tayari na walimu waendelee kuwa na subira kwani Halmashauri ya Jiji imechukua jukumu hili na wasichangishe wazazi bila kibali kutoka halmashauri," alisema.

Awali, mmoja wa wazazi, Juma Othman, alidai kuwa baada ya kutitia kwa vyoo vya wanafunzi, kila mzazi alitakiwa kuchangia Sh. 15,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo. "Hii ni elimu bure kweli? Inakuwaje tuchangishwe ujenzi wa vyoo? Sisi uwezo wetu ni kutoa nguvu kazi, siyo fedha kama uongozi wa shule unavyokubaliana katika kikao cha pamoja," alilalamika.

Nipashe ilitinga ofisini kwa Ofisa Elimu wa Shule ya Msingi, Joseph Mabeo, lakini hakutaka kuzungumzia lolote badala yake alitoka na kuelekea kwenye shule hiyo.

"Sihitaji kupigwa picha bila idhini yangu, nitakwenda kuangalia tatizo shuleni hapo, " alisema.

**HALI ILIVYO KITAIFA**

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2015/16, ilibainisha uhaba mkubwa wa samani na miundombinu katika shule za msingi nchini.

Katika ripoti yake hiyo, CAG anasema hali ya miundombinu na samani za shule za msingi nchini si nzuri na haikidhidhi matakwa ya viwango vya ubora.

CAG abainisha kuwa wakati idadi ya wanafunzi kwenye shule za msingi nchini ikiwa ni milioni 8.34 kwa shule za serikali mwaka huo na kiwango kinachotakiwa ni wavulana 25 kwa tundu la choo na wasichana 20 kwa tundu, Tanzania kwa sasa tundu moja linatumiwa na wavulana 57 huku wasichana 56 wakitumia tundu moja la choo.

Kwa kiwango hicho cha ubora kinachotakiwa kisera, Shule ya Msingi Ipagala inapaswa kuwa na vyoo vya wanafunzi vyenye matundu yasiyopungua 40.

## Jafo apeleka kicheko kwa wanafunzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(Tamisemi), Selemani Jafo, ameagiza kuanza kwa mchakato wa kusajili shule shikizi ya Chiwondo jijini Dodoma, ili kuwaondolea adha wanafunzi kutembea umbali wa kilometa 20 kila siku kwenda Shule ya Msingi Chihoni.

Shule hiyo kwa sasa ina wanafunzi 169 wa darasa la awali hadi la tatu huku wanafunzi wa darasa la nne hadi la saba wakiendelea kutembea umbali huo kufuata elimu.

Jafo alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizindua madarasa mawili ya shule hiyo shikizi yaliyojengwa na Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji hilo kwa ajili ya kutatua adha hiyo. Tayari vyumba vinne vya madarasa vimekamilika na vitatu bado vinajengwa.

Alisema ni hatari kwa wanafunzi wadogo kuendelea kutembea umbali mrefu kufuata elimu, akifafanua kuwa inasababisha kushindwa kufanya vizuri na wengine kuacha shule.

"Namwagiza Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, kukamilisha ujenzi wa madarasa na pia namwagiza Mkurugenzi wa Elimu Tamisemi, kuongeza madarasa mengine mawili kabla ya kuanza Bunge lijalo la bajeti.

"Huu ni mwisho wa wanafunzi kutembea umbali mrefu, usajili ukamilike mwakani ili darasa la nne na la saba wafanye mtihani hapa hapa Chiwondo na hii shule isajiliwe kwa jina la 'Shule ya Msingi Mavunde'," aliagiza.

Kuhusu upungufu wa walimu kwenye shule hiyo ambayo kwa sasa wanafunzi hao wanafundishwa na walimu wawili, Waziri Jafo aliagiza kibali cha ajira kitolewe ili walimu waongezwe kwenye shule hiyo usajili utakapokamilika.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo (katikati), akikata utepe kuzindua shule mpya ya msingi Mavunde, iliyopo Kata ya Nala, jijini Dodoma juzi. Wengine ni Mbunge wa Jimbo la Dodoma, Anthony Mavunde (kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi (kulia), na mdau wa elimu, Aisha Msantu. **PCHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wafanyabiashara wa barabarani sasa kutimuliwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imeanza operesheni ya kuwaondoa wafanyabiashara wadogo wanaofanya biashara zao kwenye maeneo yasiyo rasmi ikiwamo kwenye barabara, kwa kuwa ni maeneo hatari kiusalama na kiafya.

Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna, aliyasema hayo jana alipozungumza na viongozi wa wafanyabiashara hao kuhusiana na kampeni endelevu ya kuwaondoa wale wote wanaopanga biashara zao katika maeneo yasiyo rasmi jijini.

Alisema maeneo kama barabara za magari na watembea kwa miguu, darajani na mitaro ni hatari kwao na wateja huku akiwataka kufanya biashara kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya biashara hizo badala ya kuvamia maeneo yasiyo rasmi kwao.

Aliwataka viongozi kushirikiana na jiji kutoa elimu ili kuondoa tatizo la kufanya biashara holela bila mpangilio wowote.

"Wengi wao wamepanga biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi kama vile katika mitaro ya maji, madarajani na barabarani. Ninachowaambia, Halmashauri ya Jiji kamwe haitakubali kuona sheria na kanuni zinapuuzwa, ni muhimu wakajiondoa wenyewe kabla mali zao hazijaharibiwa na kusababisha hasara kubwa kwao," alionya.

Ofisa huyo pia aliwataka wafanyabiashara kufanya biashara kwenye masoko yaliyotengwa katika kata karibu zote kwa kuwa nafasi bado zinapatikana.

Katibu wa Wafanyabiashara hao, Victar Sijila, alisema kuwa na vitambulisho vya machinga isiwe sababu ya kukiuka sheria na kanuni zilizowekwa na halmashauri kwa kufanya biashara holela bila mpangilio.

Alisema uongozi wao unaunga mkono operesheni ya kuwaondoa wale wote wanaokiuka sheria na kanuni kwa kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi.

Katibu huyo alisema baadhi ya wafanyabiashara hao wanapanga bidhaa zao kwenye maeneo hatarishi na hakuna sababu ya kukaidi kuondolewa kwenye maeneo hayo ambayo si rasmi kwao kufanyia biashara.

Mweka hazina wa wafanyabiashara hao, Enjoy Mlemwa, aliwataka wamachinga kuwa waadilifu katika kazi kwa kuheshimu mipaka ya maeneo wanayofanyia biashara.



## Zanzibar yatakiwa kuhakiki wapangaji wenye sifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Shirika la Nyumba Zanzibar umeshauriwa kufanya uhakiki wa mikataba ya wapangaji wake ili kujua wale wenye sifa za kuendelea kupangishwa nyumba hizo kwa ajili ya kulipa kodi halisi.

Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa, Asha Abdalla Mussa, wakati akichangia kamati ya bajeti ya Baraza la Wawakilishi.

Alisema imebainika wapo wapangaji wa shirika hilo ambao wanadaiwa zaidi ya Sh. bilioni moja ikiwa ni malimbikizo ya kodi za nyumba kwa zaidi ya miaka mitatu nyuma.

Kadhalika alisema uchunguzi umebaini kwamba wapo wapangaji wanaotambuliwa na Shirika la Nyumba, lakini kwa bahati mbaya nao wamezikodisha kwa watu wengine kwa kiwango kikubwa cha fedha.

"Bado uongozi wa Shirika la Nyumba la Zanzibar haujajipanga vizuri kuliendesha shirika hilo na kufanya tathmini ikiwamo ukaguzi wa mali zake," alisema.

Alisema shirika hilo linakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo uchakavu wa majengo ambayo yalijengwa baada ya Mapinduzi ya Januari 12, mwaka 1974 ikiwamo majengo ya maendeleo ya Michenzani, Kikwajuni pamoja na Kilimani.

"Nyumba nyingi zinazomilikiwa na Shirika la Nyumba zinahitaji matengenezo makubwa na kwa bahati mbaya halina uwezo kwa sababu limeshindwa kudhibiti mali zake," alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani Pemba, Mussa Foum Mussa, alilitaka shirika hilo kudhibiti mapato ambayo yataliwezesha kuzifanyia ukarabati nyumba zake za Pemba.

Alisema nyumba nyingi za Shirika la Nyumba ziliopo Pemba zipo katika hali mbaya na kutoa mfano wa nyumba za Kengeja ambazo tayari baadhi ya wananchi wamelazimika kuzihama.

"Nyumba za Shirika la Nyumba ziliopo Pemba zipo katika hali mbaya zinahitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa ili kuzinusuru na maisha ya wapangaji wake," alisema.

Nyumba hizo zilijengwa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar Hayati Abeid Amani Karume, baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni ahadi ya kuwawezesha wananchi kuishi katika makazi mapya.

Alisema nyumba za maendeleo kwa upande wa Pemba zimejengwa Micheweni, Chakechake, Mkoani, Wete na Kengeja mkoa wa kaskazini Unguja.

# Shein ataka programu kupata walimu wa sayansi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein ameitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwa na programu maalum ya mafunzo itakayowezesha kuwa na walimu wa kutosha wa masomo ya sayansi ili kuondokana na upungufu wa walimu wa kada hiyo.

Akipokea taarifa ya utekelezaji ya mpango kazi wa wizara hiyo, Ikulu Mjini Zanzibar, alisema ni vyema wizara ikaandaa utaratibu wa muda mfupi utakaowawezesha wahitimu wa sekondari waliofaulu masomo ya sayansi na wanaomaliza shahada katika vyuo vikuu nchini, kujiunga katika mafunzo hayo na hatimaye kupelekwa katika shule mbalimbali.

Alisema katika kipindi cha miaka 56 tangu Mapinduzi ya 1964 ya Zanzibar, siyo jambo jema kwa Zanzibar kubaki na tatizo la upungufu wa walimu wa sayansi na kuendelea kutegemea walimu kutoka nje ya nchi.

Alieleza kuwa wizara hiyo ni ya kitaaluma na yenye watendaji weledi na wenye uzoefu, hivyo ni vyema wakajipanga ili kumaliza kabisa kadhia hiyo iliyodumu kipindi mrefu.

Aliitaka wizara hiyo kuandaa na kutuma waraka maalum serikalini kuhusu azma ya kuwa na maktaba mpya ya kisasa itakayojikita katika matumizi ya mitandao.

Pia kupitia sekta tofauti Zanzibar imeanzisha majengo mbalimbali ya kisasa na kuwapo umuhimu wa kuwa na maktaba ya kisasa ili kuchochea maendeleo ya kielimu nchini.

Rais Dk. Shein, alitaka wizara hiyo kuangalia uwezekano wa kuwa na shule mbili zaidi za wasichana mikoani, kutoka miongoni mwa shule tatu zinazoendelea kujengwa, ili kufanya jumla ya shule nne za wasichana kwa Unguja na Pemba.

Alisema kuna umuhimu wa kuwapo utaratibu maalum wa kuwafikia wananchi wasiojua kusoma na kuandika katika shehiya mbalimbali nchini, ikiwa ni hatua ya kuondokana kabisa na jamii isiyojuwa kusoma na kuandika.

Kadhalika Dk. Shein alitaka umuhimu wa kufanya utafiti kwa mustakbali wa maendeleo ya elimu nchini na uongozi wa wizara hiyo kukaa na kufikiria namna ya kuwa na taasisi ya elimu na utafiti.

Awali, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alisema wizara hiyo imepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mpango wa elimu wa mwaka 2019/2020, hatua iliyokwenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya CCM ya 2015-2020.

Alisema miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya kidato cha nne 2019 katika daraja la kwanza, pili na la tatu.

Alisema katika kipindi hicho idadi ya watahiniwa waliofaulu daraja la kwanza walikuwa 299, ikilinganishwa na watahiniwa 185 waliofaulu katika mitihani ya 2018.

Waziri Pembe aliyataja mafanikio mengine yaliyopatikana katika kipindi hicho kuwa ni mwendelezo wa ujenzi wa vituo 22 vya ubunifu wa sayansi Unguja na Pemba, vinavyotarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa bajeti.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (kulia), akizungumza na Uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango, katika kikao cha utekelezaji mpango kazi kwa kipindi cha Julai-Desemba 2019, kilichofanyika katika ukumbi wa Ikulu, mjini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Utitiri wa kodi sekta ya utalii walalamikiwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi imesema imebaini kuwapo utitiri wa kodi kwa wawekezaji wa sekta ya utalii.

Akisoma ripoti ya kamati hiyo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Mwenyekiti wa Kamati, Mohamed Said Dimwa, alisema kuna kodi zinazokusanywa na taasisi za ukusanyaji wa mapato, lakini kuna kodi nyingine zinakusanywa na halmashauri hali inayoleta usumbufu kwa wawekezaji hasa wamiliki wa hoteli za kitalii.

Alisema katika kuweka mazingira bora ambayo hayatawakwaza wawekezaji na serikali kukusanya kodi, kamati inaishauri serikali kuimarisha mfumo wa ukusanyaji mapato.

Alisema ni vyema kuziunganisha kodi na tozo mbalimbali ambazo mwekezaji anatakiwa kuzilipa ili kuokoa muda, gharama na usumbufu. Mwenyekiti huyo alisema changamoto hizo zinazotokana na uratibu wa ukaduzi wa mizigo bandarini ambazo zinawapa usumbufu mkubwa wafanyabiashara na kuingia gharama za uhifadhi wa mizigo kutokana na kuchelewa kutolewa mizigo yao. Alisema kuwapo kwa hali hiyo, kamati ililitisha kikao cha pamoja na kuzikutanisha taasisi zote zinazohusika na ukaguzi wa mizigo bandarini na taasisi hizo zilikiri kuwapo kwa changamoto katika uratibu wa ukaguzi wa mizigo bandarini.

Alisema kamati inapendekeza utaratibu au mwongozo uliopo ambao unaotumika kufanyiwa mapitio na kurekebishwa ili kontena za bidhaa zisizofaa kwa matumizi yasiachwe kukaa bandarini kwa muda mrefu bila ya kutozwa malipo yoyote.

Akizungumzia kuhusu uwekaji wa kamera na vifaa vya ulinzi, alisema changamoto za kutokamilika kwa mradi zinaweza kusababisha kutokuwa endelevu kwa siku za usoni licha ya kuwa fedha nyingi zimetumika.

Alisema miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na tatizo la kutofanya kazi kwa kamera zilizowekwa katika baadhi ya maeneo. "Kamati inaishauri serikali kuimarisha mawasiliano na ushirikiano baina ya taasisi za serikali wakati wa kuanza utekelezaji wa miradi ili kuepusha utekekezaji wa mradi mmoja kuharibu miundombinu ya miradi mengine na kuibebesha serikali gharama zisizo za lazima.

# Bashe azipa somo kampuni za bima

**Na Enock Charles**

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amezitaka kampuni za bima za mazao nchini kuboresha bima za mazao kwa kuweka bidhaa za bima zinazoendana na mahitaji ya sasa ya wakulima.

Lengo ni kuwainua wakulima wenye mitaji midogo kufikia hali bora ya kiuchumi ikiwamo kuweka bidhaa za bima zinazofika hadi katika masoko badala ya kuishia shambani.

Akizungumza na kampuni za bima jijini Dar es Salaam, wakati wa kikao kati ya kampuni hizo, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na wadau wa kilimo, Bashe alisema bidhaa za bima zilizopo hazifikii mahitaji ya mkulima ikiwamo uhakika wa masoko na kiwango cha riba kulingana na aina ya zao analolima.

"Bidhaa za bima zisiishie shambani tu zifike hadi katika masoko, bima zote zinaongozwa na kitu kinaitwa 'endemit principles' kwamba mtu kumrudisha pale alipokuwa," alisema Bashe.

"Lazima tuwe na bidhaa ambazo zinajibu mahitaji ya mkulima, mkulima anakopeshwa, mazao yake yanachukua muda mrefu na grace period (muda wa matazamio) ambayo mkulima anapewa labda ni miezi 12 tu hii haiwezekani," alisema.

Alisema licha ya suala la bima katika kilimo kuwa jambo geni nchini, lakini likiboreshwa litakuwa na faida kubwa kwa mkulima kuliko ilivyo sasa ambapo kampuni nyingi za bima zinaiga mfumo wa bidhaa uliofanikiwa katika nchi za Ulaya akieleza kuwa mazingira ya nchi hizo yanatofautiana kwa kiasi kikubwa na mazingira yaliyopo nchini.

"Kwanza, tunataka mkulima akopesheke, lakini anakopesheka kwa riba gani kwa mfano, leo hii wewe kama unalima zao kama parachichi mkulima analima na mpaka anavuna tunda ni miaka mitatu, lakini benki inapompa mkopo bidhaa za mikopo za benki nyingi zimedizainiwa katika mfumo wa kama biashara ya duka," alisema Bashe.

Naye Meneja Miradi wa TADB), Wende Mengele, alisema, benki hiyo inaamini kuwekeza katika kilimo na kwamba kwa ushirikiano na wadau wa kilimo ikiwamo bima za mazao ya kilimo changamoto zilizopo katika sekta ya kilimo zinaweza kutatuliwa na kumwezesha mkulima kukopesheka kwa urahisi.

"Kwa kuzingatia kuwa asilimia 70 ya wananchi wamajishughulisha katika kilimo tupo na kampuni za bima ili kuhakikisha hizi huduma zinamfikia mkulima kwa gharama nafuu," alisema Wende.



Ofisa Mwandamizi wa Equinor Tanzania, Dk. Naomi Makota (katikati), akikabidhi mabati yenye thamani ya Sh. milioni 10, kwa Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Lindi, Maggid Myao (kushoto), kwa ajili ya msaada kwa wananchi walioathirika na mafuriko mkoani humo, jana. Kulia ni Ofisa Mawasiliano wa Equinor, Erick Mchome. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakala wa mbegu walia miundombinu

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WAKALA wa Mbegu Tanzania (ASA,) unakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji ambayo ingewasaidia kuongeza uzalishaji, na kuwa na mbegu kwa wakati wote.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mtendaji Mkuu wa wakala wa mbegu Tanzania (ASA), Dk. Sophia Kashenge, alisema licha ya sasa kulima huku wakiendelea kuuza mbegu, lakini wangepata kilimo cha umwagiliaji wakalima kila wakati, wangeweza kuwa na mbegu nyingi.

Alisema kilimo cha umwagiliaji kingewasaidia kuwa na mbegu nyingi ambazo zingefanya upatikanaji wa mbegu katika mashamba yao yote tisa nchini na kuwa na uhakika wa wingi wa mbegu na kufanya serikali kuzuia uingizwaji wa mbegu kutoka nje ya nchi. Aidha, aliipongeza serikali kwa kufanikiwa kununua matrekta matatu ya zana za kilimo za kufanyia shughuli mbalimbali nchini mwaka jana yenye thamani ya Sh. bilioni moja kupitia ASA.

Dk. Kashenge alisema awali ASA walikuwa na matrekta matatu pekee ambayo hayakuwa na uwezo zaidi ya kulima na kulazimika kukodisha ndege za kumwaga dawa wadudu wanapozagaa shambani ili kulinda mbegu.

Dk. Kashenge alisema kwa sasa matrekta hayo matatu yenye zana zake zenye uwezo wa kumwaga dawa ya kupandia, mawili na la kupigia haro moja yanawasaidia katika mashamba tisa ya mbegu wanayomiliki yaliyopo mikoa mbalimbali nchini.

Aidha, alisema pamoja na changamoto wanazopitia, bado wanaongeza uzalishaji ambapo mwaka 2018/19 waliweza kuzalisha tani 1,220 za mbegu za mazao mbalimbali wanayozalisha na kufanya ongezeko la tani 784.

Alisema kwa mwaka 2018/19 walizalisha tani 1,436 za mbegu kupitia uzalishaji wa mawakala wao wa kilimo kwa kampuni nane wanzofanya nazo kazi kwenye mashamba yao nchini ambapo mwaka 2017/18 walizalisha tani 2,500 na kufanya uwepo wa tani 3,936 za mbegu.

Dk. Kashenge alisema mpango wa ASA ni kuzalisha tani 4,400 za mbegu mbalimbali kwa hekta ambayo ni sawa na ekari mbili na nusu kwa mwaka.

# Zaidi waibuka kidedea droo NBC Malengo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imeendelea kuboresha maisha ya wateja wake kwa kuendelea kutoa zawadi mbalimbali kupitia kampeni yake inayoendelea ya akaunti ya Malengo iitwayo 'Ibuka Kidedea na NBC Malengo'.

Akizungumza wakati wa droo ya mwezi Januari katika droo za kila mwezi za kampeni ya Ibuka Kidedea jijni Dar es Salaam jana, Meneja Masoko wa NBC, Alina Maria Kimaryo, alisema kampeni hiyo imeendelea kufanya vizuri tangu ilipozinduliwa Oktoba mwaka jana, ikishuhudia wateja wa zamani wakiweka amana katika akaunti zao za Malengo, huku wateja wapya wakijiunga na NBC Malengo ili kujishindia zawadi na kunufaika na manufaa lukuki yanayopatikana sambamba na akaunti hiyo.

"Tunaposema 'Ibuka Kidedea' ni kweli tunamaanisha, kwani mjuavyo hadi sasa jumla ya washindi 10 wamejishindia zawadi za bodaboda huku washindi nane wameshinda safari za mapumziko kwenda sychelles na Serengeti.

"NBC Ibuka Kidedea imekuja kusaidia Watanzania kutimiza malengo yao. Watanzania wana malengo mbalimbali kila mmoja ana malengo yake, natoa wito kwa wateja wetu na wasio wateja kujiunga na NBC Malengo ili kutimiza malengo yenu kwa urahisi na uhakika," alisema Maria.

"Tunajua fika mahitaji halisi ya Watanzania, tunajua mahitaji ya wateja wetu, akaunti ya Malengo ya NBC ni moja ya fursa iliyoletwa na NBC ili kumuwezesha mteja wetu kujiwekea akiba kidogo kidogo ili kutimiza malengo yake. "Tunataka wateja wetu na Watanzania wawe na utamaduni wa kujiwekea akiba hata kama ni kidogo kidogo kwani mswahili wanasema 'bandu bandu humaliza gogo," alisema.

Alisema wanaojiunga na NBC Malengo sio tu kupata nafasi ya kuibuka kidedea, lakini wanashuhudia akaunti zao zikipata faida nono kila mwezi hivyo kuwasaidia kutimiza malengo yao.

Katika droo ya jana Wahindi watano waliibuka kidedea na kujishindia pikipiki mpya aina ya Yamaha kila mmoja, huku zawadi kubwa ikipangwa kuwa pikipiki ya miguu mitatu aina ya Toyo itakayotolewa katika droo kubwa inayotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

Mbali na droo hiyo pia mshindi wa droo ya Desemba mwaka jana, Rosemary Kibodya wa Dar es Salaam, alikabidhiwa pikipiki yake katika tukio lililoshuhudiwa pia na wakaguzi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania.

## HABARI KIMATAIFA

### Undugu wa Uganda, Rwanda wazidi kunoga

**KIGALI,** Rwanda

MARAIS wa Uganda na Rwanda wanatarajia kukutana kesho katika mpaka wa Uganda na Rwanda katika eneo la Katuna katika juhudi za kuendeleza mchakato wa kuimarisha uhusiano wa nchi hizo mbili, ambao ulikuwa unalega lega.

Raia wa pande zote mbili wanatarajia kuwaona marais hao wakifungua mpaka wa Gatuna uliofungwa Februari mwaka jana na kurudisisha uhusiano mwema wa mataifa hayo.

Rais wa Rwanda, Paul Kagame na mwenzake Yoweri Museveni wa Uganda wamekuwa wakikutana na kuafikiana kuhusu kuimarisha uhusiano kati yao ili kumaliza uhasama uliopo.

Wiki hii Serikali ya Uganda iliwaachia huru raia wengine 13 wa Rwanda waliokuwa wamezuiliwa katika jela zake wakituhumiwa kwa makosa mbalimbali.

Kwa mujibu wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Uganda, Sam Kutesa, raia hao wa Rwanda ni wale waliokamatwa mwaka 2019 kwa makosa mbalimbali yakiwamo ya kukutwa na silaha.

Hili ni kundi la pili baada ya Wanyarwanda wengine kukabidhiwa mwanzoni mwa Januari, 2020, katika hatua ya kumaliza uhasama uliopo kati ya mataifa hayo. **RFI**

### Al Shabab washambulia Kenya, Somalia

**MOGADISHU,** Somalia

WANAMGAMBO wa kundi la Al Shabab kutoka Somalia wametekeleza mashambulio mawili dhidi ya kambi kadhaa za kijeshi huko Qoryoley, kilomita 30 Magharibi mwa Mogadishu.

Idadi ya watu waliouawa katika mashambulizi hayo haijajulikana lakini silaha kadhaa ziliibwa, kulingana na vyanzo kadhaa kutoka Somalia.

Shambulio la pili lilitokea saa chache baada ya shambulio la kwanza dhidi ya kambi nyingine ya jeshi katika mazingira yanayofanana, huko Ceel-Salini, kilomita 30 kutoka eneo ambalo kumetokea shambulizi la kwanza.

Ofisa katika Jeshi la Somalia ameliambia Shirika la Habari la AFP kwamba washambuliaji hao walitimuliwa kwa msaada wa Kikosi cha Jeshi la Umoja wa Afrika nchini Somalia (AMISOM).

Wanamgambo hao pia wametekeleza shambulizi lingine baya dhidi ya basi la abiria lililokuwa likitokea Mandera likielekea Nairobi nchini Kenya na kwamba abiria watatu waliuawa.

Tangu mwanzoni mwa mwaka huu, wanamgambo wa Kiislamu wa kundi la Al Shabaab wameongeza mashambulizi mbali na mpaka wa Somalia katika juhudi za kuonyesha kuwa bado wana nguvu katika ukanda huo. **RFI**

# Corona yapiga hodi Iran, watu wawili wafariki dunia

**TEHRAN,** Iran

IRAN imethibitisha vifo vya watu wawili vilivyotokana na maambukizi mapya ya virusi vya corona na kuvifanya kuwa vifo vya kwanza kuripotiwa eneo la Mashariki ya Kati.

Wakati vifo hivyo vikiripotiwa Iran, maambukizi nchini China yanaendelea kupungua ingawa wataalamu wanaonya kwamba virusi hivyo vinaweza kuenea zaidi kuliko ilivyodhaniwa.

Maofisa wa afya nchini Iran, walithibitisha kutokea kwa matukio mawili ya maambukizi mapya ya virusi vya corona vilivyopewa jina la COVID-19, kwamba wanaume wawili wazee wamepoteza maisha katika mji wa Qom.

Shirika la habari la Iran IRNA, limesema shule na vyuo huenda vikafungwa katika mji huo wa Qom kwa ajili ya kufanya uchunguzi.

**Idadi ya vifo nchini China imefikia watu 2,118 baada ya watu wengine 114 kufariki, lakini maofisa wa afya wameelezea kiwango kidogo cha maambukizi mapya kulinganisha na hapo awali.**

Vilevile imeanza kuchukua hatua za tahadhari hususani katika viwanja vya ndege ambako abiria tofauti wanawasili.

Vifo hivyo ni vya kwanza kuripotiwa katika eneo la Mashariki ya Kati. Kwingineko watu tisa wameripotiwa kuwa na maambukizi ya corona katika nchi ya Umoja wa Falme za Kiarabu.

Idadi ya vifo nchini China imefikia watu 2,118 baada ya watu wengine 114 kufariki, lakini maofisa wa afya wameelezea kiwango kidogo cha maambukizi mapya kulinganisha na hapo awali.

Zaidi ya watu 74,000 wameambukizwa virusi hivyo ndani ya China na mamia wengine katika nchi zaidi ya 25. Wakati China ikishuhudia kupungua kwa maambukizi ya mlipuko wa COVID-19, serikali ya Japan imekabiliwa na ukosoaji juu ya hatua za kuiweka katika uangalizi meli ya Diamond Princess. Siku ya Jumatano abiria 500 waliondolewa ndani ya meli hiyo baada ya kubainika kutokuwa na maambukizi ya corona.

Wakati huo huo, wanasayansi wa China wanazijaribu dawa mbili za kupambana na virusi hivyo na matokeo ya awali yatatolewa wiki ijayo.

Daktari Marie-Paule Kieny ambaye ni mtaalamu wa zamani wa maradhi ya mlipuko kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) alifanya utafiti wa siku mbili mjini Geneva wa wanasayansi zaidi ya 300 wakiwamo kutoka China na Taiwan.

Dk. Kieny amesema bado haijafahamika ikiwa tiba hiyo itathibitisha ufanisi dhidi ya virusi vipya na kwamba hawajui matokeo hivyo wanapaswa kusubiri kwa siku kadhaa.

Korea Kusini nayo imeripoti maambukizi mapya 31 ya corona na kufanya idadi ya walioambukizwa kufikia 82. **DW**



Wapiganaji wa kikundi cha waasi cha Idlib nchini Uturuki wakitekeleza mashambulio nchini humo. **PICHA: AP**

# Mbunge atinga bungeni na nzige

**KAMPALA,** Uganda

MBUNGE wa Jimbo la Ngora Mashariki mwa Uganda, David Obala, alitinga ndani ya bunge akiwa amebeba nzige.

Lengo la kubeba wadudu hao ambao wamekuwa tishio kwa sasa ni kupinga hatua ya serikali ya kuchelewa kulianga-zia janga la kukabiliana na mlipuko wa wadudu hao ambao wameharibu mimea katika eneo la Afrika Mashariki, hatua inayozua hofu ya kusababisha ba la njaa.

Hatua ya Obala kuingia na nzige bungeni kulizua gumzo katika mitandao ya kijamii baada ya video yako kusambaa.

Muda mfupi baadaye, mmoja wa wabunge alilalamika kwa spika hali iliyomlazimu Obala kuikabidhi chupa iliojaa nzige kwa ofisa wa bunge anayesaidia kutuliza vurugu bungeni.

Obala alidai kuwa Spika alipaswa kuelezewa kila wiki kutoka kwa wizara kuhusu hatua ya serikali ya kuwanyunyuzia dawa wadudu hao kisha naye kutoa taarifa bungeni.

Gazeti la Daily Monitor nchini Uganda lilituma ujumbe kwenye mtandao wa kijamii wa twitter ikionesha video ya mbunge huyo akionekana akiwabeba nzige hao ndani ya bunge.

Kulingana na Daily Monitor, tayari serikali imenunua lita 10,000 ya dawa ya wadudu hao ambayo hutumika kote duniani kwa unyunyizaji wa dawa angani.

Dawa hiyo inatarajiwa kuwasili nchini humo Ijumaa kutoka nchini Japan, kulingana na maofisa katika Wizara ya Kilimo.

Wadudu hao wamedaiwa kusambaa katika wilaya 17 nchini Uganda ikiwamo Acholi, Karamoja, Teso na maeneo yaliopo Magharibi mwa Mto Nile.

Wilaya zingine ni Abim, Kaabong, Nakapiripirit, Amudat, Agago, Katakwi, Nabilatuk, Moroto, Kitgun, Soroti na Kole miongoni mwa maeneo mengine. **BBC**

# Hatima ya Halima Mdee Aprili Mosi

**Na Hellen Mwango**

HATIMA ya Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, anayekabiliwa na kesi ya uchochezi kujulikana Aprili Mosi kama ana kesi ya kujibu au la.

Hatua hiyo imefikiwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, baada ya upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wao.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kusikilizwa, lakini upande wa Jamhuri umefunga ushahidi wao na kwamba mashahidi watatu wanatosha kujenga kesi yao.

Hakimu Simba alisema upande wa utetezi uwasilishe hoja zao ndani ya siku 14 na upande wa Jamhuri uwasilishe majibu baada ya siku 14 nyingine.

Alisema mahakama yake itatoa uamuzi wa kama kigogo huyo wa kitaifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mdee ana kesi ya kujibu au la Aprili Mosi.

Mapema mahakamani hapo, mashahidi watatu wa upande wa Jamhuri wametoa ushahidi akiwamo Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Urafiki, Mrakibu wa Polisi (SP) Batseba Kasanga.



Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Julai 3, 2017 katika Makao Makuu ya Ofisi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), iliyopo Mtaa wa Ufipa Wilaya ya Kinondoni, Mdee anadaiwa kutamka maneno dhidi ya Rais John Magufuli kuwa "anaongea ovyo ovyo, anatakiwa afungwe breki" kwamba kitendo ambacho kingeweza kusababisha uvunjifu wa amani.

Mdee alifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza na kusomewa mashtaka yake Julai 10, 2017 na yupo nje kwa dhamana.



Mtaalamu wa Huduma za Kidigitali wa Tigo, Ikunda Ngowi, akizungumza na wanahabari, jijini Dar es Salaam juzi, katika uzinduzi wa promosheni ya 'Bid-2-Win' au Toa bei Ushinde, itakayowapa wateja nafasi ya kununua bidhaa mbalimbali kwa bei ya chini na kujishindia zawadi zenye thamani ya hadi Sh. milioni 5. Kushoto ni Mtaalamu wa Huduma za Ziada, Fabian Felician.
**PICHA: JOHN BADI**

# Mkandarasi umeme apewa hadi Feb. 28

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amemtaka mkandarasi wa kampuni ya KEC International Limited anayetekeleza mradi wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme katika kituo cha Zuzu jijini Dodoma kukamilisha kazi hiyo ifikapo Februari 28, mwaka huu.

Kituo hicho hadi kukamilika, kitakuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 640. Kalemani alitoa kauli hiyo jana, alipofanya ziara kwa mara ya tatu katika kituo hicho kwa lengo la kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo.

Dk. Kalemani (pichani) alifafanua kuwa mradi huo ni muhimu kwa Watanzania hasa wakazi wa Dodoma kwa kuwa baada ya kukamilika kwa kituo hicho, kitakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati zaidi ya 600, na kuwa kituo cha kwanza nchini kuzalisha umeme kwa wingi.

Hata hivyo waziri huyo alisema, serikali haiwezi kuvumilia uzembe na uwekaji wa vibarua wachache.



"Nawataka mwongeze vibarua, hili agizo nalitoa mara ya pili leo, nataka niwaongezee mpaka mwezi Machi... hili haliwezekani, mradi ulipaswa kukamilika na ikifika Februari 28 muwe mmekamilisha, la sivyo nitaondoka na watu hapa, lazima tutachukua hatua, siwezi kukubali Watanzania walale gizani," alisema Kamwelwe.

Waziri alibainisha kuwa baada ya kukamilika kwa kituo hicho, kitakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 600, zikijumuishwa na megawati 48 zinazozalishwa kwa sasa jumla zitakuwa 648, zikitumika 40 watabaki na akiba ya megawati 608.

"Sasa Dodoma italipita hata Jiji la Dar es Salaam ambalo linaongoza kwa sasa kwa kuwa na megawati takribani 587, napenda niishukuru sana serikali kupitia kwa Mheshimiwa Rais kwa kutupatia Dola za Marekani milioni 52 kwa ajili ya kutekeleza mradi huu," alisema.

Kuhusu manufaa ya mradi huo, Dk. Kalemani alisema mbali na kutosheleza mahitaji ya kawaida ya wananchi, kiasi hicho cha umeme pia kitawezesha uwekezaji wa viwanda vya aina mbalimbali, hivyo kukuza uchumi.

Katika hatua nyingine, waziri huyo ameuagiza uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kupitia kwa Msimamizi wa Mradi husika, Mhandisi Peter Kigadye, kushughulikia malalamiko ya wananchi wanaoishi jirani na kituo hicho na kuunganishiwa huduma ya umeme na kuboreshewa miundombinu ya barabara.

# Jela miaka 30 kwa unyang'anyi

**Na Daniel Limbe,** CHATO

MKAZI wa Kijiji cha Murusagamba wilayani Ngara mkoani Kagera, Mussa Behe (26), amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 jela baada ya kupatikana na hatia ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Mshtakiwa huyo ambaye alikuwa na wenzake wawili, Mussa Abdul na Wasola Maduka, wanadaiwa kufanya vitendo vya unyang'anyi baada ya kumjeruhi kwa kisu kisha kumfunga kamba Kurwa Shabani, mkazi wa Chato mjini.

Katika kesi hiyo namba 22 ya mwaka 2020, Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Mauzi Lyawatwa, alidai kosa hilo linaangukia kwenye Kifungu cha 287(A) cha Sheria ya Makosa ya Jinai Sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Alidai Januari 20 mwaka huu, mshtakiwa (Behe) alimkodi Kurwa Shabani, ambaye ni mwendesha bodaboda kutoka Kijiji cha Muungano kwenda Kijiji cha Kisesa wilayani humo.

Lwawatwa alidai kuwa pasipo kujua kama mteja wake ana nia ovu, akiwa na pikipiki yenye namba za usajili MC 115 CDH, mwendesha bodaboda huyo alimbeba mteja wake hadi Kijiji cha Kisesa, eneo ambalo lilikuwa na vichaka.

Alidai kuwa katika vichaka hivyo, mteja wake alimwamuru kusimama, na kwamba kando ya eneo hilo kulikuwa na vijana wawili waliojitokeza ghafla na kuanza kumshambulia mwendesha bodaboda huyo.

Mwendesha mashtaka huyo alidai kuwa mbali na kipigo alichokipata, majeruhi huyo alijifanya kuzirai na ndipo watu hao walipomfunga kwa kamba na kumwacha eneo hilo wakiamini wamekwishamuua kisha wakatokomea na pikipiki aliyokuwa nayo.

Alidai kuwa baada ya wanyang'anyi hao kutokomea, majeruhi huyo (Shaban) alianza kupiga yowe kuomba msaada kwa wasamalia wema ambao walifika na kuanza kuwafuatilia wahalifu hao na kufanikiwa kuwakamata wawili huku mmoja akitokomea kusikojulikana.

Baada ya kusomewa mashtaka yaliyokuwa yanawakabili, Mshtakiwa wa Kwanza, Mussa Behe, alikiri kutenda kosa hilo huku mshtakiwa wa pili, Mussa Abdul, akikana kuhusika na unyang'anyi huo.

Baada ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Chato, Odira Amworo, kusikiliza maelezo ya pande zote mbili na kwa kuzingatia mshtakiwa wa kwanza alikiri kwa kinywa chake kutenda kosa hilo, alisema mahakama hiyo ilimhukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 jela ili liwe fundisho kwa wengine.

HABARI KITAIFA

# 'Maji bado shida kwa wanawake'

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

SERIKALI imeombwa kuboresha miundombinu ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa maeneo ya pembezoni hususani vijijini ambako kwa kiasi kikubwa huchota maji ya kwenye visima, ambayo siyo safi wala salama.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Mkoa wa Singida, Happy Francis, alitoa ushauri huo kwenye Kongamano la Kanda ya Kati kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mkoani Singida.

Alisisitiza pia kwamba licha ya upatikanaji wa maji katika eneo la kanda hiyo ni ya shida sana.

Hata hivyo, aliipongeza serikali ya awamu ya tano kwamba kwa kiasi fulani imejitahidi kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa maji.

Happy alisema pamoja na serikali kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa maji kwenye maeneo mengi ya mijini, lakini bado kuna maeneo mengi ya pembezoni yanayokabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma hiyo ya maji.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, mwanamke wa maeneo ya vijijini mwenye hali ya chini bado hutumia muda wake mwingi kwa kutembea umbali mrefu kutafuta maji na kutokana na kitendo cha umbali huo wa upatikanaji wa maji, hashiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Usafi wa Mazingira (SUWASA) Singida, Mhandisi Patrick Nzamba, alisema kuwa hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kitaifa imefikia asilimia 71 ambapo maeneo ya vijijini ni asilimia 34 na maeneo ya vijiji yamefikia asilimia 67.

# Matatani madai ya kuchenjua dhahabu kwa kutumia sumu

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

WATU wawili wa familia moja, mpangaji na madereva wawili wa bajaji wanashikiliwa na Jeshi la Polisi wilayani Kahama kwa tuhuma ya kufanya shughuli za uchenjuaji wa dhahabu inayohusisha sumu katika makazi ya wananchi.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Majengo, Vicent Asenga, akithibitisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao alidai kuwa tukio hilo limetokea jana majira ya saa saba mchana katika familia ya Frank Peter, mkazi wa Kata ya Majengo Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga.

Alidai kuwa wanafamilia hao wanafanya shughuli hiyo bila kujua athari zitakazowapata wananchi wa eneo hilo kutokana na sumu wanayotumia katika uchenjuaji dhahabu.

Asenga aliwataja walioshikiliwa na polisi kwa ajili ya mahojiano maalumu kuhusiana na tuhuma hizo kuwa ni pamoja na Frank Pius, Lucy Pius, mpangaji wao Ally Mohamed na madereva wawili waliokutwa wanahamisha vifaa hivyo ili kupoteza ushahidi.

"Kwa Kata ya Majengo ni tukio la pili, mimi nikiri kwamba huyu mtu anafanya shughuli hizo bila kibali cha serikali, lakini haya ni maeneo ya makazi ya wananchi uongozi wa kata tumekuwa tukitoa elimu kuhusu sumu inayotumika katika uchenjuaji wa dhahabu jambo ambalo linahatarisha maisha ya wananchi kwa kuwa sio waelewa," alisema.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Joseph Kumburu, akizungumza na waandishi wa habari katika eneo la tukio, alisema Februari 18, mwaka huu majira ya saa saba mchana alimkamata Lucy na Frank kwa kosa la kuendesha shughuli za uchenjuaji wa dhahabu katika makazi ya wananchi.

Alisema kukamatwa kwa watuhumiwa hao ni kutokana na mtego uliowekwa na ofisi ya madini Kahama na mmoja wa maafisa kutoka Ofisi ya Madini Mkoa wa Kahama, alibaini kuwapo kwa hali hiyo na mtuhumiwa huyo alikutwa akifanya shughuli za uchenjuaji nyumbani kwake huku akijua ni kosa kisheria na anafanya kazi hizo bila kibali.

Alisema wakiendelea na ukaguzi katika vyumba vitano katika nyumba hiyo, pia vilikutwa vifaa vya uchenjuaji na madumu mawili ya sumu ya kunasia dhahabu na vifaa vingine kwa ajili ya shughuli hiyo katika chumba cha Ally Mohamed, jambo ambalo ni hatari kwa afya zao wenyewe na wananchi wanaowazunguka.

"Watuhumiwa hao kwa sasa wapo polisi kwa mahojiano zaidi, lakini tumekamata madereva wawili waliokuwa wakitorosha vifaa hivyo pamoja na mpangaji huyo naye atueleze anahusikaje na vifaa vya madini vilivyokuwa ndani mwake," alisema Mhandisi Joseph Kumburu.

Kufuatia tukio hilo Ofisa Madini huyo aliwapiga marufuku wananchi kuendesha shughuli za uchenjuaji wa madini katika maeneo ya makazi ya wananchi ili kuepuka madhara yanayotokana na maji ya sumu kutiririka katika makazi ya wananchi.

Hata hivyo kwa upande wake, Frank Simon, alipotakiwa kuzungumzia tuhuma hizo zinazomkabili, alidai kuwa vifaa hivyo ni kwa ajili ya shughuli zake za madini na alikuwa amevihifadhi ndani kwa kuwa havikuwa na kazi kwa wakati huo na kukiri kujihusisha na shughuli za uchenjuaji wa dhahabu huku akidai kuwa anafuatilia kibali na kwa sasa anatumia vibali vya wanunuzi wa dhahabu (MADIRA).

Katika sakata hilo vimekamatwa vifaa mbalimbali ambavyo ni pamoja na lita 40 za maji ya dhahabu, steel wire, copper wire, kemikali za kunasia dhahabu, kinu cha dhahabu, jiko kwa ajili ya kuchomea dhahabu carbon kilo 200 zinazosadikiwa kuwa na dhahabu, mkasi wa kushikilia dhahabu na vitu vingine vingi.



Baadhi ya watu wenye ulemavu waliohudhuria kongamano katika mikoa ya Dodoma, Tabora na Singida wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi (hayupo pichani). **PICHA: JUMBE ISMAILLY**

# Kampuni ununuzi pamba zafagiliwa kwa bei elekezi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Annamringi Macha, amepongeza kampuni za ununuzi na uchambuzi wa zao la pamba wilayani hapa, kwa kununua zao hilo kwa Sh. 1,200 licha ya kuwa na mtikisiko wa bei duniani.

Macha aliyasema hayo juzi wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Kahama ya Uchanguzi Mkuu wa 2015 katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2019 ambapo alisema serikali inaendelea kutatua changamoto za wakulima kwa kufuatilia madai yao na kuwatafutia masoko.

Alisema kuwa katika kampuni zilizofanya vizuri katika ununuzi wa zao la pamba ni ya mzawa ya Kahama Oil Mill (KOM) iliyonunua kilo 890,680 zenye thamani ya Sh. bilioni 1.06.

Aidha, alisema kuwa, Kampuni ya Fresho pia ilinunua kilo 2,931,930 yenye thamani ya Sh. bilioni 3.5, hali ambayo iliwafanya wakulima kutokuwa na malalamiko mengi kuhusu suala la bei katika msimu uliopita.

Macha lisema katika kipindi cha mwaka 2015/2019, baadhi ya vikundi 283 katika Halmashauri ya Mji wa Kahama walipewa mikopo ya kilimo na kulima mazao yao ya chakula na biashara katika maeneo yao na kupunguza wimbi la vijana mitaani. Alisema kuwa katika kipindi cha mwaka 2019/2020, jumla ya vikundi 29 vilivyolima ekari 195 na kupewa pembejeo za kiasi cha Sh. milioni 17.9 vilifanikiwa na kupata faida katika mazao waliokuwa wakilima na kujipatikia kipato kwa ajili ya kuendesha familia zao.

Hata hivyo, Macha alisema Wilaya ya Kahama kwa sasa ina vyama vya msingi vya ushirika 116 ambavyo kwa msimu wa mwaka 2018/19 vilinunua kilo milioni 4.5 za pamba zenye thamani ya shilingi bilioni 5 na kilo milioni 10 za tumbaku zenye thamnani ya dola za kimarekani milioni 14.2 (sawa na shilingi bilioni 33).

Mbunge wa Msalala, Ezekiel Maige, alisema kuwa serikali inatekeleza miradi kwa kutumia fedha ambazo hupitishwa bungeni ni kila mwaka wa fedha.

Alisema kuwa Halmashauri ya Msalala imepokea zaidi ya shilingi bilioni 41.6 kwa ajili ya kuekeleza na kukamilisha miradi ambayo haijakamilika ikiwamo mradi wa maji na kuongeza haijawahi kutokea Msalala kupokea mradi na fedha nyingi kiasi hicho.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NYUMBA INAUZWA MIL 70 ARUSHA NGULELO:,** SELF VYUMBA 3 KIMOJA MASTER, SITTING, JIKO NA STORE, INA UMEME âNA MAJI INAFAA KUISHI, FINISHING NA FENSI UNAIMALIZIA. MWENYE NYUMBA **0757 804 970**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


## KUPOTEA KWA CHETI



**GEORGE S LYIMO** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba PO321/0173 Kilichotolewa na Baraza La Mitihani La Taifa Kupitia KINONDONI SECONDARY SCHOOL mwaka 2000

Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi KL/MOS/RB/152521/2020

156399

## KUPOTEA KWA PASPOTI



SAID ABDALLAH MOHAMED amepotelewa na paspoti ya kusafiria yenye namba AB 881718 na Yenye RB namba MOR/MOR/RB/94715/2020.

156401

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 35/2020**

Ombi la **HAKAI IBRAHIM TINDO** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MARIAM RASHID MUSSA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 26/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 12/02/2020.

HAKIMU

115638402

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF ILEMELA**
**AT ILEMELA**
**CIVIL CASE NO 10/2019**
**ELIAS MASATU MAYAGI............PLAINTIFF**
**VRS**
**1. WADDOCK SACCOSS LTD...... DEFENDANTS**
**2. DKT SEVERINE M .LALIKA**

**NOTICE OF DATE OF MENTION/HEARING**

**TAKE NOTICE THAT**; the above case has been fixed for **HEARING on 20th day of FEBRUARY 2020**

**YOUR ARE** required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to reply upon in support of your case.

**GIVEN UNDER** my hand and the SEAL of the court this 10 day of **JANUARY 2020 at 08:30 AM.**

RESIDENT MAGISTRATE

115638302

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ABDALLAH HEMED HASSAN** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye namba za usajili MC 822 BXZ na MC 479 BXY zote aina ya Bajaj Boxer.

**Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi: DAR/OST/RB/149784/2020.**

156386

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MOSHI**
**WILAYA MOSHI**
**MAOMBI NA. 126/2018**
**MICHAEL KITIMBWA CHUWA NA WENZAKE**
**............WALETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**FREDRICK KIZITO KIROMBOLE CHUWA**
**.......MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

KWA : FREDRICK KIZITO KIROMBOLE CHUWA
POPOTE ULIPO

Kwa kuwa waleta maombi wameleta madai ya kesi na yameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la ardhi na Nyumba Moshi .Shauri limepangwa kutajwa tarehe 24/02/2020 saa mbili na nusu (2:30)asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti J. SILLAS, hivyo unatakiwa kufika mahakamani wewe au wakili wako

ANGALIA: Kama hutahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 24 mwezi Octoba,2019

MWENYEKITI

156396

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya mwanzo**
**Hai Kati**
**Usimamizi wa mirathi namba 13 mwaka 2019,**

Ombi la Cuthbert E Urassa kuteuliwa msimamizi wa mirath marehemu Elias Stephano Urasa.

Kwa yeyote anaehusika Tanzania Bara,

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhuthuria kesi wakitaka mnao tarehe 05-08-2019 kabla huyu mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa .

Imwtokea leo tarehe 22-07-2019 mwaka 2019

SAHIHI YA HAKIMU

156397

---

**JAMUHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**
**Mahakama**
**Usimamizi wa mirathi**
**(S.M.M 1984 Nyongeza ya 5 kanuni 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo Dodoma**
**Usimamizi wa mirathi 16/2020**
**Ombi la SHANI SALUM MASHAKA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi marehemu JUMANNE SALUM**

Kwa yeyote anauehusika Tanzania Bara.

Watu wote wanaodai kuwa na mahusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 27/2/2020. Kabla ya mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 02/02/2020.

Sahihi ya Hakimu

115639402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;57/2020**
**Ombi la GRACE AVINARY MANDE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu YASINTA EDWARD MAIKO.**

**Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.**

**Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 20/02/2020**

HAKIMU

156390

## KUPOTEA KWA KADI

Christopher Andrew Mlay anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA COROLA yenye namba za usajili T805 ANY , Yenye chassis namba EE1110004129 na Injini namba AE1492833 Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi MOS/TR/RB/237/2020

156400

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;49/2020**

Ombi la AZIZA YUSUPH KISYUKA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu YUSUPH KONDO KISYUKA.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 28/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/02/2020.

HAKIMU

156389

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo -**
**MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;51/2020**

Ombi la GISELA BALTAZARY Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu TWALIBU SHABAN.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 27/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 18/02/2020.

HAKIMU

156393

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 55/2020**

Ombi la **TAMASHA HAMIM LUVAKO** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **BASHIRU YASINI BUTOKI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 19/02/2020.

115638502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DAIS MARION SINTALA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili **No T 216 ANV** Chassis No. **MR053AN5000063192.** Engine No **5AJ034113.** Kwa atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi **ARU/ARU/RB/160581/2020.**

215638702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SADICK RAJAB KALERANDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T. 931 BEE aina ya SUZUKI rangi nyeupe CHASSIS namba SAFTD62V00109730

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi MBE/MBE/RB/161170/2020.

115639202


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Mourinho: Dele Alli akasirikia kiwango

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amesisitiza Dele Alli alikuwa na hasira na kiwango chake mwenyewe, si maamuzi ya kumtoa nje, baada ya kuonyesha ghadhabu wakati akitoka nje ya dimba Tottenham ikifungwa bao 1-0 na RB Leipzig kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora.

Alli alionekana kushangaa wakati alipotakiwa kutoka nje ya dimba dakika ya 64 pale kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur, na alionekana kutupa chupa ya maji kwa hasira.

Hata hivyo, Mourinho alikataa madai kwamba Alli alikasirishwa na maamuzi ya kutolewa na alisisitiza wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari kwamba, kutolewa kwake kulikuwa sehemu ya kuimarisha zaidi kiwango cha Tottenham.

“Nafikiri alikuwa na hasira na kiwango chake, si dhidi yangu mimi,” alisema Mourinho. “Nafikiri anaelewa kwa nini nilimtoa nje, na timu iliimarika.”

Alli hakuwa kwenye kiwango bora kwenye mchezo huo dhidi ya Leipzig ambao walitawala kipindi cha kwanza na bao lao lilifungwa na Timo Werner kwa mkwaju wa penalti baada ya Ben Davies kumfanyia madhambi Konrad Laimer eneo la hatari dakika ya 58.

Spurs awali walikuwa kwenye wakati mzuri, lakini umakini mdogo wa wachezaji wake Giovani Lo Celso, Erik Lamela na Lucas Moura ukawafanya washindwe kusawazisha bao na kuongeza.

Na Mourinho alionyesha wazi kwamba, kukosekana kwa Heung-Min Son na Harry Kane walio majeruhi kumechangia kikosi chake kutokuwa na kasi kubwa katika mchezo huo.







# MKE HAJUI KAMA ICARDI ATABAKI PSG

**PARIS,** Ufaransa

WAKALA na mke wa Mauro Icardi, Wanda Nara hajui kama nyota huyo atabakia Paris Saint-Germain ambako anacheza kwa mkopo au atarudi kwenye klabu yake ya Inter Milan wakati huu akihusishwa na mpango wa kwenda Juventus.

Icardi anacheza kwa mkopo kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, PSG, ambao wana kipengele kinachowawezesha kumnunua moja kwa moja kwa euro milioni 70 mwisho mwa msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alikuwa hatakiwi na kocha wa sasa wa Inter, Antonio Conte ambaye alianza kuiongoza klabu hiyo mwanzoni mwa msimu huu na akachukuliwa kwa mkopo kule PSG ambako amefunga mabao 19 kwenye mashindano yote.

Icardi, ambaye amefunga mara mbili katika mechi 12 zilizopita, awali aliripotiwa kwamba anataka kubakia hapo PSG, lakini Nara amesema hana uhakika kuhusu majaliwa ya mume wake huyo.

“Mauro atakwenda Juventus? Kwa uhakika kabisa sijui,” alisema Nara akiliambia Jarida la Chi.

“Sijui kama msimu ujauo atarudi Milan au atabakia Paris. Kwenye soka huwezi kujua lolote linaweza kutokea.

“Yeye atachagua na sisi tutamfuata. Ni ngumu kusema kwa sasa, sababu namjua sana Mauro na kwa uhakika kabisa najua nini anachotaka kama mwanasoka na nini kinachomfanya ajisikie vizuri.”

## *Kocha ambakisha Van de Beek Ajax*

**AMSTERDAM,** Uholanzi

KOCHA wa Ajax, Erik ten Hag ana matumaini kiungo nyota wa klabu hiyo, Donny van de Beek atabakia klabuni hapo licha ya kutakiwa na Real Madrid na Manchester United.

Van de Beek ameendelea kuhusishwa na mpango wa kutakiwa na miamba hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Madrid, ambao awali waliwasiliana na Ajax juu ya uwezekano wa kumsajili nyota huyo mwanzoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 nyota wa kimataifa wa Uholanzi, pia amekuwa akihusishwa kutakiwa kwenye Ligi Kuu ya England pale United.

Ten Hag alipoulizwa na waandishi wa habari kuhusu majaliwa ya Van de Beek kuelekea kwenye mchezo wa jana Alhamisi wa Ligi ya Europa dhidi ya Getafe mjini Madrid, alijibu: “Sidhani kama ataondoka.”

“Ni mchezaji wa kiwango cha juu na sisi tusingependa kumpoteza licha ya kutakiwa na timu kadhaa.”

Ten Hag aliongeza: “Donny van de Beek amekuwa na maendeleo mazuri zaidi kwa miezi michache iliyopita. Klabu nyingi kubwa zimekuwa zikimfuatilia.



# RONALDO: HUYU MBAPPE ANATISHA




**PARIS,** Ufaransa

CRISTIANO Ronaldo amemsifia nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe kama ni mchezaji mzuri wa soka wa sasa na wa baadaye.

Mbappe alijiimarisha yeye mwenyewe kuwa mmoja ya wachezaji bora duniani baada ya kung'ara kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, wakati akiwa pale Monaco msimu wa 2016-17.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, tayari ameshinda Kombe la Dunia na mataji matatu ya Ligue 1, na matatu mengine ya nyumbani akiwa na Ufaransa, PSG na Monaco.

Akiwa anaendelea kuhusishwa na mpango wa kutua kwa miamba wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Real Madrid na Juventus ya Italia, mshindi mara tano wa Ballon d'Or, Ronaldo amemwaga sifa nyingi kwa Mbappe.

"Mbappe ni wa baadaye na sasa," amesema Ronaldo kupitia video aliyoiposti kwenye ukurasa wa gazeti la Marca.

"Ni mchezaji anayevutia, ana kasi sana na atakuwa bora zaidi wa baadaye."

Akionekana kama ndiye mrithi wa Ronaldo na nyota wa Barcelona, Lionel Messi, Mbappe amejiimarisha zaidi mwenyewe pale PSG.

# Guardiola: Siondoki City, labda nifukuzwe

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesisitiza atabakia Manchester City msimu ujao licha ya klabu hiyo kufungiwa misimu miwili kushiriki michuano ya Ulaya.

Kumekuwa na hofu kwamba Guardiola na baadhi ya wachezaji wanaweza kutafuta sehemu nyingine ya kwenda kama City haitapunguziwa adhabu ya kufungiwa miaka miwili ya kushiriki michuano ya Ulaya baada ya kuvunja sheria ya fedha ya Uefa.

Lakini baada ya City kuibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya West Ham kwenye Ligi Kuu ya England juzi Jumatano, raia huyo wa Hispania amebainisha kwamba bado ana muda mrefu wa kuendelea kukaa na klabu hiyo, ambayo imesema itapigana hadi tone la mwisho kupinga adhabu hiyo ya Uefa.

"Binafsi, bila kujali lolote litakalotokea nitakuwa hapa msimu ujao," alisema Guardiola akiiambia Sky Sports.

"Kama Klabu haitanifukuza mimi, hilo linaweza kutokea nitabakia hapa kwa asilimia 100 na zaidi ya hapo.

"Kwanza kwa sababu nataka kubakia hapa zaidi ya mkataba wangu nilionao. Ni kitu fulani maalumu, nataka kubakia, nataka kuisaidia klabu, kama inawezekana, kuendelea kuifanya klabu iwe kwenye kiwango kilekile.






# Messi: Neymar anataka kurudi tena Barca

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi amesema Neymar anataka kurudi Barcelona, huku mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or akisifia ripoti za klabu yake kutaka kumsajili nyota wa Inter Milan, Lautaro Martinez.

Neymar aliondoka Barca kwenda Paris Saint-Germain kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222 katika uhamisho wa mwaka 2017, lakini nyota huyo wa Brazil ameendelea kuhusishwa na mpango wa kurejea Camp Nou.

Mshambuliaji huyo wa PSG ameripotiwa kwamba amekuwa alijaribu kulazimisha uhamisho wa kurudi Barca mwanzoni mwa msimu, ingawa uhamisho huo ulishindikana, licha klabu hiyo kujaribu mara kadhaa.

Messi, ambaye hajaficha siri ya kutaka kuungana na Neymar, ameliambia gazeti la Mundo Deportivo: "Nimesema mara nyingi, Ney ni mmoja wa wachezaji bora duniani na ningependa arudi hapa.

"Kwa uhakika mshambuliaji anataka kurudi, mara zote amekuwa anajisikia vibaya baada ya kuondoka. Alifanya mengi ili arudi na hiyo itakuwa hatua nzuri zaidi kama akirudi tena hapa."

Uamuzi wa Neymar kuondoka Barca miaka mitatu iliyopita uliwakasirisha baadhi ya wachezaji wenzake, lakini Messi alisema: "Ni kawaida kwa watu kumwangalia kwa namna hiyo kwa sababu kwa namna alivyoondoka, hata mimi ilinihuzunisha wakati ule, tulijaribu kumshawishi asiondoke.

"Lakini mwisho wa siku wote tulitaka kushinda na kuwa bora. Kama nilivyosema awali yeye ni mmoja wa wachezaji bora uwanjani.

"Lakini inaeleweka namna watu wanavyofikiri, kwa staili aliyoamua kuondoka wengi hawakuipenda."

Barca pia imekuwa ikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan, Martinez akionekana kama ndiye mrithi wa muda mrefu wa Luis Suarez.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RASHFORD KUMALIZA MSIMU NJE - SOLSKJAER

Asema kuna uwezekano pia kuikosa Euro 2020 kama...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amesema Marcus Rashford atakaa nje ya uwanja kwa muda mrefu zaidi kuliko ilivyotarajiwa awali kutokana na majeraha yake ya mgongo.

**Solskjaer amesema ni "gusa na kuondoka" ikiwa Rashford atakuwa sawa vya kutosha kurudi kabla ya mwishoni mwa msimu na ameonya kwamba anaweza kukosa michuano ya Euro 2020.**

Rashford anasumbuliwa na majeraha ya mgongo aliyoyapata baada ya kutokea benchi wakati Manchester United ikishinda 1-0 dhidi ya Wolves katika mechi ya Kombe la FA Januari 15, mwaka huu.

Awali kulikuwa na matumaini angekuwa nje kwa takriban wiki sita, lakini sasa anakabiliwa na kukaa nje zaidi, na Solskjaer amekiri hakuna uhakika kamili wa lini Rashford atakuwa fiti vyakutosha kurejea.

"Natumai atacheza msimu huu. Itakuwa kugusa tu na kwenda kuelekea mwisho," alisema kabla ya Manchester United kushuka dimbani jana kuivaa Club Brugge kwenye michuano ya Europa League.

"Tunatumai tutavuka michuano hii na kuuendeleza msimu huu. Itachukua muda, mimi si daktari. Nilitumai angepona haraka kuliko kama inavyoonekana sasa itakavyokwenda kuwa kwa miezi mingine michache dhahiri.

"Kama hatakuwa fiti vya kutosha hatakwenda [michuano ya Euro]."

Wakati alipoulizwa kwa nini muda ulioelezwa awali kwamba Rashford atarejea umeongezeka, Solskjaer aliongeza: "Alifanyiwa vipimo na alikuwa na majeraha makubwa kuliko tulivyotarajia. Alijisikia vizuri siku chache kabla ya hapo.

"Sikujua itamchukua muda huo kupona. Wakati akipona atakuwa imara kwa hilo, hivyo ni muhimu hatutaliharakisha na hatutalifanya hilo."

## ZISIKUPITE

### RONDON AIOTA MAN UNITED

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Newcastle United, Salomon Rondon, 30, anaamini Manchester United ilitoa ofa ya kumsajili dakika za mwisho kabla ya dirisha kufungwa kutoka Dalian ya Ligi Kuu China. ***(AS, via Star)***

### ARSENAL HESABU KWA TAH

ARSENAL inavutiwa na beki wa Bayer Leverkusen, Mjerumani Jonathan Tah, 24, ambaye atapatikana kwa pauni milioni 33.4 kipindi cha majira ya joto. ***(Bild - in German)***

### UNITED TAJIAMINI KWA SANCHO

MANCHESTER United inaamini itamsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, 19, katika majira ya joto, lakini lazima kwanza ifuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Sky Sports)***

### AHOFIA KUIKOSA LIVERPOOL

MSHAMBULIAJI wa RB Leipzig, Timo Werner, 23, amesema alijisikia "fahari" kuhusishwa na Liverpool lakini anahisi hatakuwa tayari kujiunga na kwa kile anachozingatia kuwa "timu bora duniani". ***(Metro)***

### MESSI AITWA LA GALAXY

MSHAMBULIAJI wa Barcelona na Argentina, Lionel Messi, alipigiwa simu na LA Galaxy kujadili suala la kujiunga na klabu hiyo ya Ligi Kuu Marekani, MLS. ***(Express)***

### JESUS, ICARDI WAWINDWA

JUVENTUS imeainisha kuwa mshambuliaji wa Manchester City, Mbrazil Gabriel Jesus, 22, na wa Paris St-Germain, Muargentina Mauro Icardi, 23, kama wachezaji inaowawinda kuelekea usajili wa majira ya joto. ***(Tuttosport - in Italian)***

### ARSENAL, EVERTON ZATUA GENT

ARSENAL, Everton na Leicester City ni miongoni mwa klabu saba zinazovutiwa kumsajili mshambuliaji wa Gent na Canada, Jonathan David, 20. ***(Jeunes Footeux, via Sun)***

### MAWINDONI KWA MERTENS

MIAMBA ya Serie A, Inter Milan itaingia mawindoni kuisaka saini ya mshambuliaji wa Napoli, Mbelgiji Dries Mertens, 32, katika dirisha la majira ya joto. ***(Calciomercato - in Italian)***

### JUVE YAJIPANGA KWA POGBA

HATUA ya Manchester United kutaja dau la kiungo wake, Mfaransa Paul Pogba, 26, inamaana Juventus inajipima uzani wa kuipiku Bayern Munich huku kiungo Mhispania Thiago Alcantara, 28, akiwa kama mbadala. ***(Tuttosport, via Mail)***

### LIVERPOOL KUMFUATA RASHICA

LIVERPOOL inapanga kumsajili kiungo wa Werder Bremen na Kosovo, Milot Rashica, 23, ambaye anaruhusiwa kuvunja mkataba wake kwa pauni milioni 31.5. ***(Bild, via Mirror)***

### YAMFUNGUKIA BELLINGHAM

CHELSEA ipo tayari kumsajili kiungo wa Birmingham City, Muingereza Jude Bellingham, 16, hata hivyo dau la pauni milioni 50 zinazohitajika zitaathiri kumaliza na kiungo Faustino Anjorin, 18, kwa mkataba wa muda mrefu. ***(Sun)***

# Michezo

Ijumaa Februari 21, 2020

Nipashe





Rashford kumaliza msimu nje - Solskjaer

UKURASA 27

PAMOJA SANA...




Mshindi wa Jackpot ya SportPesa wa zaidi ya Sh. milioni 437, Yassin Ridhiwani (mwenye kofia nyeupe) ambaye ni mshabiki wa Yanga, akiwa katika picha ya pamoja na wachezaji wa timu hiyo baada ya kupata nafasi ya kuwatembelea kambini wiki iliyopita jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Yanga yaichambua Coastal ikitafuta 3

## ●●● Kocha asema ni ngumu ila pointi tatu ni muhimu, Mgunda aonya akidai...

**Na Saada Akida**

HUKU wakiwa na kibarua kigumu cha kufuta mzimu wa sare unaowaandama, Kocha Msaidizi wa Yanga, Boniface Mkwassa amesema mchezo dhidi ya Coastal Union ni mgumu ila wamejipanga kupata pointi tatu kesho.

**Yanga inashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kupata sare ya tatu mfululizo baada ya Jumanne katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, kuambulia alama moja kutokana na mchezo dhidi ya Polisi Tanzania kumalizika kwa bao 1-1.**

Matokeo hayo yalikuja ikiwa ni baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City kisha zikafuata dakika 90 za suluhu dhidi ya Tanzania Prisons, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Lakini itakutana na Coastal Union iliyotoka kujeruhiwa nyumbani na Ruvu Shooting kwa mabao 2-1 Jumanne wiki hii.

Akizungumza na mwandishi wetu jana kwa njia ya simu kutoka Tanga, Mkwassa alisema pamoja na kutambua ugumu wa mchezo huo, watajitahidi kuibuka na alama tatu.

"Coastal ni timu imara, ipo vizuri, ukizingatia kwamba haijawa na mwenendo mbaya kwenye ligi, tunatambua mchezo utakuwa mgumu ila tumejipanga kufanya vema na kuona namna gani tutapata pointi tatu," alisema Mkwassa.

Alisema licha ya mshambuliaji wao, Tariq Seif kupatwa na majeraha katika mechi iliyopita, jana aliweza kufanya mazoezi na wenzake, hivyo bado hawajajua mchezaji ambaye anaweza kuukosa mchezo huo.

"Hatujafanya mazoezi magumu, ni ngumu kujua nani atakosa, lakini suala la Tariq kuwapo au kutokuwapo ni mapema mno hadi hapo atakapofanya mazoezi ikiwa ni pamoja na daktari kumfuatilia na kutupa taarifa zake na majeruhi wengine," alisema Mkwassa.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda alisema wamejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huo dhidi ya Yanga ili kuhakikisha wanawaongezea majeraha kwa kutoondoka na alama yoyote Mkwakwani.

"Tunajiandaa kucheza na Yanga, si majina makubwa ya wachezaji wao, tunawaheshimu na tunahitaji kupambana kusaka alamu tatu katika mchezo wetu huo," alisema Mgunda.

# Jembe Simba larejea mzigoni

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, uongozi wa klabu hiyo pamoja na mashabiki wakikunwa na uwezo wa kikosi hicho kwa sasa, 'jembe' lao tegemeo limerejea mzigoni likitokea chumba cha majeruhi.

Katika mechi tatu zilizopita; dhidi ya Mtibwa Sugar Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro Simba ikishinda 3-0 na kisha dimba la Samora Iringa dhidi ya Lipuli FC ikashinda bao 1-0 kabla ya kuibuka na ushindi kama huo Uwanja wa Taifa dhidi ya Kagera Sugar Jumanne wiki hii, vijana hao wa kocha Sven walionyesha kiwango cha kuvutia hali iliyowaziba mashabiki mdomo waliokuwa wakimponda Mbelgiji huyo.

Na tangu kumalizika kwa michuano ya Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar Januari 13, mwaka huu, Simba ilimkosa kiungo wake mkabaji, Mzamiru Yassin ambaye sasa amerejea na kuanza mazoezi na wenzake hali ambayo imeelezwa itakwenda kuzidi kukiboresha kikosi.

Akizungumza na Nipashe jana daktari wa timu hiyo, Yassin Gembe alisema mchezaji huyo kwa sasa anaendelea vizuri na anafanya mazoezi na wenzake huku winga Miraji Athumani naye akiendelea na programu ya mazoezi mepesi akiwa nyumbani.

"Mzamiru anaendelea vizuri na leo (jana), amefanya mazoezi ya asubuhi na wenzake isipokuwa Miraji Athumani yeye bado hajakaa vizuri anafanya mazoezi mepesi mepesi na baada ya wiki mbili ataungana na wenzake na mashabiki wetu wataendelea kumuona uwanjani," alisema Gembe.

Kwa upande wa Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu alisema, lengo lao ni kuendeleza ushindani kwa wapinzani wao hadi mwisho ili kuhakikisha wanatwaa ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo na kwamba itakuwa ni vigumu kupokonya ubingwa huo kirahisi kulingana na mikakati ambayo wamejiwekea.

Alisema Sven ameahidi kufanyia kazi upungufu uliyojitokeza katika mechi iliyopita dhidi ya Kagera Sugar, ambayo licha ya kuonyesha kandanda la kuvutia, safu ya ushambuliaji ilipoteza nafasi nyingi za mabao na kujikuta wakiibuka na ushindi mwembamba wa bao 1-0.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >

# Nipashe

Ijumaa Februari 21, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580160

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Mbowe: Tunawafahamu wote wanaotaka kuhama Chadema




UKURASA 13

# NMB yazindua Bancassurance

"Malengo yetu ni kuhakikisha kuwa asilimia 60 ya Watanzania watu wazima wanapata huduma za bima ifikapo mwaka 2024."

**Kamishna wa Mamlaka ya Bima nchini (TIRA), Dkt. Mussa Juma**

"Tunaamini ujio wa Benki ya NMB katika kutoa huduma za bima ni 'game changer' (inabadili mwenendo wa sekta) kuelekea viwango vya juu..."

**Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi, Biashara Ndogo na za Kati wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi**




***Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya NMB, Margaret Ikongo akipongenzwa na Kamishna wa Mamlaka ya Bima nchini (TIRA) Dr Mussa Juma muda mfupi baada ya uzinduzi rasmi wa huduma za bima kupitia benki ya NMB. Uzinduzi huo ulifanyika juzi jioni jijini Dar es Salaam.***

## Pata bima kupitia matawi 224 ya NMB Nchi nzima



Benki ya NMB imeanza kutoa huduma za bima katika matawi yake yote 224 nchini kote.

Huduma hii imefuatia uzinduzi wa huduma ya bima kupitia benki (Bancassurance) uliofanyika Jumatano jioni jiji Dar es Salaam.

**Huduma za bima zitakazopatikana katika matawi ya Benki ya NMB ni pamoja na zile za kampuni za Sanlam Life, UAP, Shirika la Bima la Taifa (National Insurance Corporation - NIC), Jubilee, Shirika la Bima la Zanzibar (Zanzibar Insurance Corporation – ZIC) na Reliance.**

Akizungumza katika uzinduzi huo, Meneja Mwandamizi wa Bima wa Benki ya NMB, Bw. Martin Massawe, alisema uwepo wa matawi ya benki yake katika wilaya zote nchini kutasaidia kukuza sekta ya bima na kuinua mchango wake katika pato la taifa.

"Tulipata leseni ya kutoa huduma za bima mara baada ya kupitishwa kwa kanuni za Bancassurance mwaka jana. Kutokana na kupatikana kwa matawi ya NMB katika wilaya zote nchini, tunaamini kupatikana kwa huduma za bima katika matawi yetu kutasaidia kukuza sekta ya bima," alisema.

Naye Kamishna wa Mamlaka ya Bima nchini (TIRA), Dkt. Mussa Juma alisema serikali kupitia taasisi yake inafanya juhudi mbalimbali ili kukuza sekta ya bima nchini ili mchango wake katika pato la taifa ufikie asilimia tatu ifikapo mwaka 2023.

Hivi sasa sekta ya bima inayosimamiwa na Mamlaka ya Bima Nchini, huchangia asilimia 0.7 ya pato la taifa.




## Kata **Bima** kupitia tawi lolote la NMB karibu yako!

Piga **0800 002 002** bure!

RELIANCE INSURANCE COMPANY (TANZANIA) LTD

Sanlam

Jubilee INSURANCE

UAP Better. Simple. Life.

NATIONAL INSURANCE CORPORATION OF TANZANIA LIMITED

SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR INSURANCE CORPORATION

www.nmbbank.co.tz




## Kata **Bima** kupitia tawi lolote la NMB karibu yako!

Piga **0800 002 002** bure!

RELIANCE INSURANCE COMPANY (TANZANIA) LTD

Sanlam

Jubilee INSURANCE

UAP Better. Simple. Life.

NIC NATIONAL INSURANCE CORPORATION OF TANZANIA LIMITED

SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR INSURANCE CORPORATION

www.nmbbank.co.tz

# “Unavimba UMEBIMA?”

## Uzinduzi wa NMB Bancassurance ulivyofana



*Msanii wa kizazi kipya Marioo akitumbuiza kwenye uzinduzi wa NMB Bancassurance jijini Dar es Salaam.*



*Mdahalo kuhusu mchango wa benki kwenye utoaji wa huduma za bima nchini.*



*Meneja Mwandamizi wa Bima NMB, Martine Massawe akiongea kwenye uzinduzi wa huduma ya NMB Bancassurance jijini Dar es Salaam.*



*Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi, Biashara Ndogo na za Kati, Filbert Mponzi (katikati) akiwa na Kamishna wa Bima kutoka Mamlaka ya Bima nchini (TIRA), Dkt. Mussa Juma (kushoto) na Meneja Mwandamizi wa Bima NMB, Martine Massawe (Kulia) wakati wa uzinduzi wa NMB Bancassurance uliofanyika jijini Dar es Salaam.*



*Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya NMB, Margaret Ikongo akipongezwa na Kamishna wa Bima kutoka Mamlaka ya Bima nchini (TIRA), Dkt. Mussa Juma baada ya uzinduzi wa NMB Bancassurance jijini Dar es Salaam. Katikati ni Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi, Biashara Ndogo na za Kati, Filbert Mponzi.*